Ijumaa Julai 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581735

MWANGA WA JAMII


LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




UK. 22

**SOUTHGATE: KUFIKA FAINALI YA MAFANIKIO YANGU**

# Maeneo haya hatari kwa afya



• **Muhimbili** yapokea wagonjwa 20 kila siku, matibabu yake yanafika hadi milioni 70/-... *Uk 2*






## Mbaroni akidaiwa kuua rafiki kisha kuchota mil. 61/- katika akaunti yake

UK. 2



Waliokuwa wafanyabiashara katika Soko la Kariakoo, wakiwa wamefunga barabara ya Lumumba, nje ya Ofisi ndogo za Makao Makuu ya CCM, jijini Dar es Salaam jana, walipofika kutoa malalamiko yao kwa viongozi wa chama hicho kuhusu sintofahamu ya majina yao kutoonekana katika orodha ya watakaorudi sokoni hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA 3

# Wafanyabiashara wa Kariakoo watikisa, watua CCM Lumumba

UKURASA WA 4

**Mbowe** ataja kiini uchumi Kilimanjaro kudidimia



UKURASA WA 4

**Kinana:** Uadilifu wenu uendane na matendo



UKURASA WA 19

**Rais** Ruto avunja Baraza Mawaziri, adai GZ wana mfadhili wa nje




**MICHEZO** YANGA SC KUANZA NA WARUNDI CAF UK.24

**KATUNI** UK.6




Mtaalamu wa Usikivu, Kizunguzungu, Matamshi na Lugha kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akizungumza katika maonyesho ya 48 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam, jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Maeneo haya hatari kwa afya yako

**Na Christina Mwakangale**

MTAALAMU wa Usikivu, Kizunguzungu, Matamshi na Lugha Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Fikiri Idd, ametoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yenye kelele, akiwataka kuvaa vifaa maalum ili kupunguza athari za usikivu.

Katika mazungumzo na Nipashe jana katika banda la MNH kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba, mtaalamu huyo alibainisha umuhimu na uwezo wa sikio katika usikivu unavyopungua kadri umri unavyosonga.

Alishauri wanaotembelea maeneo kama Soko Kuu la Kimataifa Kariakoo, jijini Dar es Salama na maeneo mengine yenye kelele, wavae vifaa maalum alivyovitaja kwa jina la 'ear plug na ear muffs' ili kupunguza athari.

Mtaalamu huyo pia alieleza umuhimu wa kiungo sikio kuwa ni miongoni mwa milango mitano ya fahamu, ikisaidia mwili kuwa na uwiano, kuimarisha matamshi, lugha pamoja na kuzuia mtu kuondokana kutokana na kizunguzungu.

Alisema katika maonesho hayo wanatambulisha huduma mpya ya kuwafanyia uchunguzi watoto tangu siku ya kwanza hadi mwezi mmoja, ili kubaini wenye changamoto waanze kupata tiba.

Idd alisema wazazi na walezi walio na watoto wenye changamoto ya usikivu huwafikisha hospitalini hapo wakiwa katika hatua ya juu ambayo ni nadra kurejesha usikivu wao.

"Kama ana shida ya usikivu, tukimgundua mapema tutamwekea kipandikizi, ambacho kitamsaidia kuwa na usikivu kwa asilimia 90. Changamoto ni kwamba watoto wanaletwa wakiwa na miaka sita au saba anakuwa ameishi na tatizo hili miaka yote hiyo.

"Tumegundua kwamba kama hospitali, kukabili changamoto ni kusaidia jamii kuanza uchunguzi wa mtoto anapozaliwa tu," alisema.

Idd alisema matibabu ya usikivu ni ghali na vifaa huagizwa nje ambapo kifaa kimoja hufikia hadi Sh. milioni 70. Serikali huchangia gharama za matibabu hayo.

"Serikali imechangia Sh. bilioni 2.6 kwa ajili ya vifaa hivyo. Lakini fedha hizo ni kwa ajili ya kuleta kifaa, bado matibabu ya kukiweka kwa mtoto, ni lazima mtu achangie," alisema Idd.

Mtaalamu huyo alisema kuwa watoto wanaochunguzwa kabla ya kufikisha miaka mitano, husaidia kuondokana na ukubwa wa tatizo kama vile kushindwa kutamka maneno na sauti isiyo na mawimbi.

Idd alishauri jamii kujenga utamaduni wa kufanya uchunguzi angalau mara moja au mbili kwa mwaka kwa kuwa kiwango cha tatizo la usikivu kinakua.

Alisema katika kliniki ya Muhimbili, kila siku hospitali hiyo imekuwa inapokea takriban watu 20 wenye matatizo hayo.

"Takwimu za mwaka 2023, utafiti unaonesha watu milioni 432 walipata tatizo la usikivu duniani kote na kati yao, milioni 34 ni watoto," alisema na kubainisha kuwa kundi kubwa ni watu wazima kwa kuwa hupuuzia jambo hilo.

"Hutakiwi kuingiza chochote masikioni hata pamba. Ndani ya sikio kuna nta inayozalishwa maalum kwa ajili ya kusafisha. Inaposogea nje ndio utumie kitambaa kujisafisha.

"Ear phone (spika za masikioni) ni sababu kubwa. Mfano, mtu kapanda daladala au bodaboda, kavaa 'ear phone' na ili asikie lazima aweke sauti kuzidi mngurumo wa chombo alichopanda au redio iliyoko ndani ya gari.

"Nenda Kariakoo, utagundua ghorofa moja kila duka kuna jenereta lake, bado muuzaji wa sumu ya panya ana spika yake, mwuzaji viwanja ana spika yake, mpigadebe hivyohivyo. Ukipima kiwango cha kelele pale ni kikubwa, huwezi kugundua ila utaathirika taratibu.

"Mfano, mwingine hapa tulipo (Sabasaba), hatuko mbali sana na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), lakini ndege ngapi zimepita na haujazisikia milio yake? Kwa sababu hapa kuna kiwango kikubwa cha kelele ndio maana hausikii chochote," alifafanua mtaalamu huyo.

Idd alisema ili kuepuka hali hiyo, vipo vifaa ambavyo watu wanaweza kuvitumia kupunguza kiwango cha kelele na kuondokana na athari zake.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa, ifikapo 2050, watu bilioni 2.5, wengi wao (bilioni moja ni vijana) watapoteza usikivu. Kati yao, milioni 700 ni kutoka kusini mwa Jangwa la Sahara. Wanahitaji huduma ya utengefu.

# Adaiwa kuua rafiki kisha kuchota milioni 61/- katika akaunti yake

**Na Romana Mallya**

WAKALA wa Forodha, Mussa Bakari, maarufu Buda (30), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalum Dar es Salam kwa tuhuma za kuua rafiki yake Abdallah Selemani, kisha kuchota Sh. milioni 61 katika akaunti ya marehemu.

Kamanda wa kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa na kuhojiwa Juni 28 mwaka huu kuhusu tuhuma hizo.

"Tulimkamata na kumhoji kwa kina Mussa Bakari, Wakala wa Forodha, mkazi wa Temeke, mkoani Dar es Salaam, kwa tuhuma za mauaji ya Abdallah Selemani ambaye alikuwa rafiki yake.

"Baada ya kumuua, alifanikiwa kuiba fedha za marehemu Sh. milioni 61 kutoka katika akaunti ya huyo rafiki yake," alisema Kamanda Muliro.

Akisimulia zaidi kuhusu tukio hilo, kamanda huyo alisema kuwa Mei Mosi mwaka huu, saa 10:20 asubuhi, huko Mbutu Kichangani, Kigamboni, pembezoni mwa barabara itokayo Cheka kuelekea Beach ya Kichangani, uliokotwa mwili wa mwanamume akiwa ameshafariki dunia.

"Baadaye mwili huo ulitambuliwa kuwa ni wa Abdallah Selemani, mkazi wa Chanika, Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam," alisema.

Kamanda Muliro alisema kuwa Mei 4 mwaka huu, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa ya kupotea kwa Abdallah zilizotolewa na mama yake, akieleza mtoto wake amepotea katika mazingira ya kutatanisha.

Alisema uchunguzi wa Jeshi la Polisi baadaye uligundua kuwa Aprili 30 mwaka huu, mtuhumiwa Mussa alikuwa na marehemu wakitumia gari namba T 928 DFY, aina ya Suzuki Kei, wakitokea Magomeni kwenda Temeke Kijichi mpaka eneo ulipokutwa mwili huo.

"Uchunguzi wa vitu mbalimbali umebaini kuwa mtuhumiwa alimuua na baadaye kwenda kutupa mwili huo pembezoni mwa barabara ulikookotwa.

"Baada ya kumuua, mtuhumiwa alichukua kadi ya benki ya marehemu na kwa nyakati tofauti alitoa fedha Sh. milioni 61 kutoka katika akaunti ya marehemu," alidai Kamanda Muliro.

Alisema chanzo cha mauaji ni tamaa ya kutaka kuiba fedha kutoka kwa rafiki yake. Mtuhumiwa atafikishwa mahakamani muda wowote.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), inawataka polisi baada ya kukamata mtuhumiwa, ama wamfikishe mahakamani ndani ya saa 24 tangu kukamatwa kwake au kumwachia huru, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, ikithibitika Bakari alihusika na mauaji ya rafiki yake huyo kwa kukusudia, adhabu yake ni kunyongwa hadi kufa.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema kuwa Jeshi la Polisi limekamata watuhumiwa 23 na pikipiki 39 zilizoibwa maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam.

"Watuhumiwa hao wamekuwa wakitumia mbinu ya kujifanya abiria na wakifika njiani hujitokeza watu wengine ambao humtishia dereva kwa mapanga, kumjeruhi na kuiba pikipiki.

"Wakati mwingine huiba pikipiki zinazokuwa zimeegeshwa nje, hutumia mbinu ya kuunganisha waya, kuwasha na kufanikisha wizi wao," alisema.

Kamanda Muliro alisema ufuatiliaji wao umebaini watuhumiwa hao baada ya kuiba pikipiki hizo, huziuza kwa gharama nafuu mikoa mbalimbali ikiwamo Singida na Dodoma (hasa jijini Dodoma).

"Tumekamata risiti za kugushi 18 za kusafirishia pikipiki za wizi, kadi 11 za usajili wa pikipiki, kadi tatu za usajili wa magari, vyeti mbalimbali vya kuzaliwa na kimoja cha ndoa, vyote vya kugushi," alisema.

Kamanda huyo pia alisema wamekamata namba za pikipiki tatu, kitabu kimoja cha bima ya magari, nyaraka mbalimbali za Mamlaka ya Mapato (TRA) na barua mbalimbali zenye nembo za Jeshi la Polisi.

Vitu vingine alitaja ni mihuri mbalimbali ya manispaa ya Kinondoni, Temeke, Ilala, TRA na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Mamlaka ya Bandari (TPA) na mhuri wa moto ulioandikwa 'United Republic of Tanzania' wenye nembo ya bibi na bwana.

Kamanda Muliro pia alikanusha taarifa ya sauti inayosambaa katika mitandao ya kijamii, ikielezea kuwapo tukio la mwanafunzi wa kike wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kutekwa chuoni huko na watu wasiojulikana, wakitumia usafiri wa bajaji kisha kupelekwa Kimara na baadaye kutelekezwa Masaki, jijini.

Alisema ujumbe huo wa sauti wamebaini ni wa miaka mitano iliyopita, hivyo habari hiyo haina ukweli.

"Tunaonya watu wanaozusha taarifa za uongo zenye lengo la kujenga taharuki au hofu kuwa kwa kufanya hivyo ni makosa," alisema.

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara Kariakoo watikisa, watua CCM Lumumba

**Salome Kitomari na Romana Mallya**

ZAIDI ya wafanyabiashara 900 wanaodai majina yao kutokuwamo kwenye orodha ya kurejea Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam, jana wamekusanyika viwanja vya Mnazi Mmoja, kudai haki yao.

Walikusanyika kwenye viwanja hivyo kuhakiki majina yao kwenye orodha kama tangazo la Shirika la Masoko Kariakoo lilivyoelekeza juzi, huku wakieleza kutoridhishwa na utaratibu huo.

Katika eneo hilo, wafanyabiashara hao walipindua meza na viti na kuandamana kuelekea Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Lumumba, wakiimba "Tunataka haki yetu."

Walidai kuwa walihamishwa katika soko hilo baada ya kuungua Julai mwaka 2021 na kupelekwa kwenye masoko mbalimbali kupisha ukarabati na ujenzi wa jengo jipya la ghorofa sita.

Ajali hiyo iliteketeza mali zote za wafanyabishara na serikali ilitenga Sh. bilioni 28 kwa ajili ya ukarabati.

Juzi, Shirika la Masoko Kariakoo lilitangaza kwenye tovuti yake kuwa timu maalum ya Ofisi ya Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam imekamilisha kazi ya kutangaza majina ya watu wenye sifa ya kupewa vibanda vya biashara katika soko hilo.

Shirika hilo lilitoa tangazo la wito kwa wafanyabiashara kwa ajili ya kutangaziwa orodha ya majina 1,806 na wenye sifa na vigezo vya kurejeshwa kwa mujibu wa tangazo hilo ni wafanyabiashara 891.

Aidha, kabla ya kamati kufika kwenye kikao kwa ajili ya kusoma majina, wafanyabiashara hao walianza kuondoka na baadaye kwenda Ofisi ya CCM Lumumba.

Akizungumza na wafanyabiashara hao jana, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, aliwataka leo kufika kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila kuanzia saa mbili asubuhi ili kuhakikisha haki ya kila mmoja inapatikana.

"Cha msingi ni kuzingatia haki zetu. Kama kuna maombi kwa serikali na sisi tutawasilisha kwa Rais Samia na yeye ndiye atakayetuambia kinachoendelea. Mkuu wa Mkoa anawapa pole na kesho (leo) kuanzia saa mbili asubuhi mtaonana naye.

"Mmekimbilia eneo salama. Mmekimbilia Chama Cha Mapinduzi (CCM) nyumbani, ninawapigia makofi kwa kukimbilia nyumbani, niwahakikishie Rais Samia hapendezwi wala kufurahishwa na jambo lolote la Mtanzania kunyang'anywa au kupokwa haki yake ya msingi.

"Hiki kitendo chote kinachoonekana si cha kiungwana hakiendi serikalini hata kwa mtu mmoja mmoja, mara zote serikali ya wilaya na mkoa tumekuwa tukitatua changamoto," alisema Mpogolo. Aidha, alisema maisha ya soko ni mtoto, baba na mama na wanatambua kuwa kuna watu wenye uwezo mkubwa na mdogo na jukumu la serikali ni kuhakikisha wanakua kiuchumi na kulea familia zao.

"Mmesema mmeleta malalamiko yenu kwa mama (Rais) yaani mlezi, mmesema hamjaridhishwa na idadi mlikuwa kwenye uhakiki wa mwanzo baadhi hawaonekani.

"Ni haki kwa mtu kujua mwenzake ametolewaje. Kama viongozi wa serikali chini ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, tutakwenda kuzingatia haki zetu kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake. Mlipopata changamoto aliwakimbilia na kwa kutambua majukumu yenu kwa kutambua mliishiwa alitoa Sh. bilioni 28, mjengewe soko jipya na kukarabati la zamani," alisema.

Juzi, Chalamila katika mkutano wa hadhara ziara ya Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, alitangaza utaratibu mpya wa wafanyabiashara kuingia sokoni humo kuwa ni kulipa madeni kwanza.

Alisema masoko mengi hayafanyi vizuri kutokana na kuvamiwa na madalali na kwamba, wapo waliojenga kwenye vibanda katika maeneo ya serikali na kusababisha migomo ya kutokulipa na sasa mkoa umeweka mkakati mzuri wa kutibu tatizo hilo. Chalamila alisema ujenzi wa soko hilo umefikia asilimia 96 na litakapokamilika wataingia wa zamani na wapya watakaohitaji na kipaumbele kitakuwa ni kulipa madeni.

Kwa mujibu wa tangazo kwenye tovuti ya shirika hilo iliyotolewa na Menejimenti, "Wafanyabiashara wanaodaiwa na shirika ambao wapo kwenye orodha hii wanajulishwa kuwa hawatarejeshwa sokoni hadi watakapolipa madeni ya kodi waliyolimbikiza kwa muda mrefu.

"Shirika linatoa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia leo Julai 10, 2024 hadi Agosti 9, 2024 kwa wadaiwa wote kukamilisha malipo ya madeni yao. Kwa wafanyabiashara wenye hoja au maoni kuhusu majina yao kutoonekana kwenye orodha ya uhakiki, "Shirika linatoa muda wa siku tatu kuanzia Julai 11 hadi 13, 2024 kuwasilisha madai yao. Maofisa wa shirika watakuwapo katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 9.00 alasiri kusikiliza na kutoa ufafanuzi kwa wafanyabiashara," ilisema taarifa hiyo.

Tangazo hilo lilitaja majina ya wafanyabisahra 212 ambao waligawanywa katika makundi sita ikiwa ni watakaokaa eneo la soko kuu, vigoli, soko dogo ndani, soko dogo mzunguko, soko la wazi na shimoni.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Kinana ataka viongozi CCM kuwa mfano malezi, maadili

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, (pichani) amewasisitiza wananchi na viongozi wanaotokana na chama hicho kuwa mfano bora wa maadili na malezi mema nchini.



Pia, amewakumbusha kuwa waadilifu kwa kauli, vitendo na mwonekano na wasikubali kuwa sehemu ya kusemwa vibaya kwa kutozingatia maadili.

Akizungumza jana mjini Mpanda, mkoani Katavi alipofungua Kongamano la Malezi na Maadili lililoandaliwa na Jumuiya ya Wazazi ya chama hicho, Kinana alisema kongamano hilo linazungumzia malezi na maadili mambo ambayo ni muhimu na hutegemeana.

"Yanaanza malezi halafu yanakuja maadili, mimi sio mwanafalsafa lakini katika vitu siamini kwamba kuna maadili mabaya, neno maadili ni neno nzuri tukiangalia vitabu vya dini vinaeleza kuwa maadili ni jambo jema," alisema.

Alifafanua kuwa, maadili yanapatikana kutokana na malezi na mafunzo na wanaofanya kazi hiyo ya kujenga malezi mema na maadili kwanza ni familia, ndio maana wanasema malezi. Pili ni jamii ambayo ina dhamana ya kujenga maadili kupitia malezi. Alisema kuna umuhimu wa kila mwananchi kuwa mwadilifu katika maisha ya kila siku kwa kuwa ni jambo linalosisitizwa katika vitabu vya Mwemyezi Mungu.

Alifafanua kuwa kazi ya CCM na serikali ni kusimamia maadili.

"Katika ngazi kuna kamati ya maadili. Ngazi ya taifa, kamati ya maadili mkoani, wilayani, kata mpaka chini na hii inadhihirisha umuhimu wa maadili. Ili tuwe na jamii bora inayojithamini na kuheshimu lazima kuzingatia maadili bora, hata serikali inasimamia maadili."

Pia, alisema kuna kamati ya taifa ya serikali inayosimamia maadili ya viongozi, hakuna kamati zingine zinazosimamia maendeleo au mambo mengine, lakini kuna kamati ya kusimamia maadili. Yote hiyo ni kudhihirisha umuhimu wa maadili.

Alisema kauli zinazotolewa na viongozi mbalimbali zinadhihirisha maadili, kukemea rushwa, mambo yasiyo mema kwa jamii na kuhimiza kujenga undugu, mshikamano na kusaidiana.

Aliongeza hata kaulimbiu za waasisi wa taifa wakiongozwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ziliakisi umuhimu wa maadili. "Hata leo tangu baba wa taifa afariki dunia miaka 28 iliyopita, lakini kauli zake zimebakia hai kwa kuwa alikuwa mwadilifu. Ndio maana hadi leo tunaendelea kunukuu kauli zake katika masuala mbalimbali. Sio viongozi wengi wa Afrika ambao wanakumbukwa na kufanyiwa rejewa kama anavyofanyiwa Mwalimu Nyerere.

Akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Ofisa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalumu, Victor Rubalagamu alisema ni jukumu la jamii kulinda maadili.

Alisema maendeleo ya utandawazi na teknolojia yasiwe sababu ya mmomonyoko wa maadili bali kiwe chanzo cha kujenga jamii bora ya sasa na baadaye.

Sabrina Majikata, mwezeshaji wa malezi ngazi ya taifa, alisema ujenzi wa maadili na malezi bora ni jukumu la wazazi na walezi.

Alisema moja ya changamoto kwa watoto ni harakati za kiuchumi ambazo husababisha wazazi na kukimbizana kutafuta fedha na kusahau jukumu la malezi. "Tumeacha watoto wanalelewa na wadada wasaidizi ambao nao baadhi yao wamepitia ukatili jambo ambalo wakati mwingine husababisha kulipiza kisasi kwa watoto wanaowalea," alisema.






# Mbowe ataja kiini uchumi wa Kilimanjaro kudidimia

**Na Godfrey Mushi**, ROMBO



MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (pichani) ametaja sababu za kufa kwa uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro kuwa ni siasa iliyoingizwa kwenye zao la kahawa.

Aidha, amesema kinachowakimbiza vijana wengi wa mkoa huo kwenda kutafuta maisha kwingine ni kutokana na serikali kuingiza siasa kwenye zao la kahawa ambalo lilikuwa roho ya uchumi.

Kutokana na sababu hiyo, amesema ni lazima watu wa Kilimanjaro wajipange upya kuwekeza katika elimu ya watoto wao, ili kuachana na utegemezi wa sasa wa kutegemea uchumi wa watoto walioko mbali.

Akizungumza jana katika eneo la Mamsera, Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro katika mwendelezo wa operesheni iliyobatizwa jina la 'Opereshеni GF', Mbowe alisema:

"Mkoa wa Kilimanjaro umekosa mfumo kamili wa kibiashara na kiuchumi wa kunyanyua kipato cha wananchi wake. Uchumi wa Kilimanjaro leo unategemea uchumi wa watoto walioko mbali.

"Uchumi mkubwa wa Kilimanjaro unategemea kitu kinaitwa kwa kiingereza 'remittance'; yaani fedha zinazotumwa kwa watoto, kwa ndugu walioko mbali na Kilimanjaro.

...Elimu yetu na ujasiri wetu wa biashara, ndio mtaji pekee wa Mkoa wa Kilimanjaro. Ndio sababu leo vijana wengi chini ya miaka 50 hawana ekari moja ya ardhi. Tumebaki na viamba vidogo vidogo vya kuzikana na kujenga nyumba za kulala."

Mbowe alisema mashamba ya wakazi wa Kilimanjaro, hayawezi kuwa tena mashamba makubwa ya kibiashara, kwa sababu watoto wameongezeka na 'viamba' (ardhi) vinagawanywa kidogo kidogo na havitoshi.

Aidha, aliendа mbali zaidi akisema kutokana na mazingira hayo ni lazima watu wa Kilimanjaro wajipange kuwekeza katika elimu ya watoto wao.

"Tuendelee kuhakikisha tunawekeza kwenye elimu ya watoto wetu na wanapata elimu bora, ili watoke wakatafute na kuendelea kusapoti huku nyumbani.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema vijana wengi nchini siku hizi, wamepoteza matumaini kwa sababu hakuna kazi, wakiamka asubuhi hakuna kiwanda wanachokwenda kufanya kazi hivyo kujipongeza kwa pombe kali na hatari ili kupunguza msongo wa mawazo.

"Wakiamka asubuhi hakuna mashamba ya kilimo, biashara ambako ameajiriwa. Wakiamka asubuhi wanaamka wakiwa hawana matumaini ya kuishi, wamepoteza matumaini."

Mtu akipoteza matumaini anaangukia kwenye kukata loku (kunywa pombe kupindukia). Lakini tu sio vijana wa kiume, ukienda nchi nzima hii, nenda Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro na Mwanza; kwenye mikoa mikubwa.

"Nimeshtuka juzi hata Muheza (Tanga), wadogo zetu wa kike, watoto wenu wa kike mama wa miaka 20, 19, 18, 17 wako barabarani wanaunza miili yao kwa Sh. 3,000.

"Hawa sio makahaba, hawa wamelazimishwa na hali mbaya ya maisha. Ukiona binti amesimama barabarani anauza mwili wake kwa Sh. 3,000 kwa siku, huyu kabla hamjamnyooshea kidole mkamuita kahaba muombeeni rehema.

Kwa sababu tumelazimishwa na umasikini, kufanya mambo ambayo nafsi haitaki lakini mwili unayafuata.

"Nyuma yangu hapa kuna Mlima Kilimanjaro, uko Rombo, ndiko kuna kahawa nyingi katika mkoa mzima wa Kilimanjaro. Leo mama zetu, bibi zangu hawa hapa unawakuta Moshi mjini wanauza soksi za mitumba. Mimi nilipokuwa mtoto sijawahi kuona machinga mtu mzima.

"Lakini siku hizi ukienda barabarani unakuta mama anauza ngogwe galoni moja, anauza pilipili hoho galoni moja, mtaji shilingi 15,000. Ameletewa wajukuu ameachiwa hapo nyumbani,umasikini unaumiza watu."

# Mramba: Huduma ya umeme imeimarika

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amesema ubora wa huduma ya umeme umeimarika nchini na kuondoa kero ya kukatika na mgawo.

Aidha, wanaendelea kuboresha huduma hiyo na kwamba ni wajibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kusimamia.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, alisema huduma za umeme ni moja ya sehemu ambayo inadhibitiwa na EWURA ambayo ameonyesha kufurahishwa na utendaji wake.

Alisema EWURA wamewezesha upatikanaji wa huduma yenyewe, bei na ubora wake, akieleza kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye bei ya chini zaidi ya umeme ikilinganishwa na mataifa jirani.

"Hatusemi kwamba ubora sasa umefikia mahali ambako hakuna shida hapana, lakini angalau huduma hiyo iko katika kiwango cha kuridhisha. Na tunaendelea kuboresha, kwahiyo ni wajibu wa EWURA kudhibiti na kusimamia," alisema Mhandisi Mramba.

Katika maeneo ya gesi asilia mamlaka hiyo imesaidia na inaendelea kutoa leseni kwa wanaojenga vituo vya (CAG) kwaajili ya magari na bajaji zinazotumia mfumo wa gesi, pamoja na vya mafuta.

Aidha, alisema jukumu lingine la EWURA ni kuhakikisha huduma inayotolewa na vituo husika zinakidhi mahitaji ya jamii. "Na sisi kama wizara wajibu wetu ni kuhakikisha EWURA anafanya kazi yake kwa mujibu wa sheria na sera zilizoko, lakini pia tunamwezesha kutekeleza majukumu yake katika mazingira yanayokubalika ndani ya sekta.

"Pia tunataka kuendelea kuwatia moyo Watanzania, ziko huduma nyingi zinazotolewa na mamlaka hii zikiwamo za kiushauri, kupokea malalamiko na ni wajibu wa EWURA kuyasikiliza na kuyafanyia kazi, pia tunampongeza kwa kazi nzuri inayoifanya," alisema Mhandisi Mramba.

Mkurugenzi wa EWURA, James Andilile alisema wameingia mkataba na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa lengo la kusimamia utendaji kazi wao ili kuboresha upatikanaji wa nishati hiyo na serikali inafanya uwekezaji mkubwa kuhakikisha sekta hiyo inaimarika.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akikagua shughuli zinazofanywa na Kiwanda cha kutengeneza nyaya cha Balochistan Group of Industry Ltd (BGI) cha Mkuranga, mkoani Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mradi ulinzi mazingira kunufaisha wavuvi

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA itanufaika na mradi wa miaka minne unaolenga kuimarisha ulinzi wa mazingira kwa wavuvi wadogo na jamii zinazowazunguka, kuimarisha uchumi wa buluu.

Mradi huo wa awamu ya pili wa 'Sustainable Ocean' unasimamiwa na Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu Denmark (Danish Institute of Human Rights).

Mshauri mkuu wa taasisi hiyo, Carol Rask, alisema hayo wakati walipotembelea Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hivi karibuni, jijini Dodoma.

Carol alisema mradi huo unaotarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka minne unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Swedish (SIDA). "Mradi huu umelenga kuimarisha ulinzi wa mazingira kwa wavuvi wadogo na jamii zinazowazunguka," alisema Carol.

Alisema katika kutekeleza mradi huo wamefanya ziara nchini, kukutana na wadau mbalimbali huku mmojawapo akiwa ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

"Tumetembelea Tanzania ili kujifunza zaidi kuhusu maeneo yanayoweza kuzingatiwa kutekeleza mradi huu, ikiwamo kukutana na wadau mbalimbali, kupata maoni yao pamoja na kuhakikisha watendaji wa serikali na sekta binafsi wanachukua hatua kuimarisha haki za binadamu kwa wavuvi wadogo.

"Pia na jamii inayowazunguka kwa kuzingatia sheria za kitaifa, sera na mipango inayohusiana na utawala wa wavuvi."

Mratibu Miradi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jovina Muchunguzi, alisema tume inaendelea na mchakato wa uandaaji wa mpango kazi wa kitaifa wa haki za binadamu na biashara, kwa kushirikiana na wadau kutoka serikalini na sekta binafsi.

"Tume imeshakutana na wadau hao na kuwaeleza hatua mbalimbali zilizofanyika za uandaaji wa mpango kazi huo," alisema Jovina. Kadhalika, alisema tume kwenye mchakato wa uandaaji wa mpango huo, eneo moja la kipaumbele ni kilimo na uchumi wa buluu ambao kuna shughuli za uvuvi.

"Eneo hili ni muhimu katika maisha ya Watanzania na katika mpango unaondaliwa," alisema Jovina.

Mradi huo utashirikiana na tume katika masuala ya mafunzo, utafiti, kuandaa miongozo ya kusimamia haki za binadamu na masuala mengine.

Ugeni huo, ulipokewa na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mohamed Khamis Hamad; Katibu Mtendaji Patience Ntwina na baadaye mazungumzo hayo kuongozwa na Jovina pamoja na Constatine Mugusi.

# Wauza vipodozi, chakula wapewa angalizo

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS), limewataka watu wote wanaofanya biashara ya chakula na vipodozi kusajili maeneo yao ili iwe rahisi kukaguliwa kwaajili ya usalama wa afya za wananchi.

Vilevile, limewataka wafanyabiashara na watumiaji kuhakikisha bidhaa wanazonunua zina nembo ya alama ya ubora.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Meneja wa TBS Kanda ya Mashariki, Francis Mapunda, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho yanayofanywa katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Alisema wanaofanya biashara ya vipodozi wanapaswa kutambua havina viambata sumu vyenye madhara kwa afya za watumiaji.

Pia, Mapunda alisema wamehudumia wajasiriamali wengi bure ambao wameshapata mafunzo ya biashara kutoka Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO).

Alisema kwenye maonesho hayo wananchi walitaka kupata elimu ya kutambua bidhaa zilizosajiliwa, zilizothibitishwa ubora na hatua za kufuata.

Pia aliwataka wenye viwanda nchini kufika TBS kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa vifaa wanavyotumia viwandani kwa ajili ya vipimo.

Wafanyabiashara hao wametakiwa kuacha kuogopa kwenda kwenye shirika hilo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao kwa kudhani gharama ni kubwa. Mapunda alisema wanaotaka ushauri wapitie SIDO, ambako wanafanyiwa tathmini na kisha kuandikiwa barua kwenda TBS na wanahudumiwa bure kwa miaka mitatu wakati wakiendelea kukua.

Alisema wananchi wamepata huduma ya kuelezwa aina mbalimbali za kaguzi ambazo zinafanywa na shirika ikiwamo ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

"Kwa hiyo kama kuna mtu anataka kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi akifika kwenye banda letu anapata maelezo namna gani atafuata taratibu ili kuagiza bidhaa zake nje," alisema Mapunda na kuongeza;

"Lakini pia, tunatoa elimu namna ya upimaji bidhaa kwenye maabara zetu na kuwasaidia watu wanaotaka kupata huduma ya ukaguzi wa vifaa ambavyo vinatumika kupimia viwandani," alisema.

Alifafanua kuwa wananchi wengi waliotembelea banda la TBS kwenye maonesho hayo walitaka kujua taratibu za kufuata ili waweze kuthibitisha bidhaa zao hatimaye waweze kutumia alama ya ubora.

Aidha, alisema wananchi wengi wamepata huduma walizozihitaji wakiwamo wengine waliotaka kufungua viwanda vyao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watoto walindwe kuwaepusha na ukatili wanaofanyiwa

**KUMEJITOKEZA** matukio ya mara kwa mara watoto hasa wanafunzi kufanyiwa vitendo vya ukatili na watu wazima.

Ukatili huo hufanyiwa wanapokuwa njiani kwenda shule au kurudi nyumbani na pia shuleni na walimu au watu wazima walio kwenye mazingira hayo.

Ukatili upo wa aina mbalimbali, lakini ulioshamiri ni wa watoto kubakwa na kuingiliwa kinyume na maumbile.

Watoto hawa sasa hawana mahali salama ambapo mzazi atakuwa na amani kama mtoto wake akitoka nyumbani atarudi salama ama la.

Wengi wa watoto hao hufanyiwa ukatili huo kwa kupata vitisho kuwa wakisema watauawa na watu wanaowafanyia ukatili huo.

Watoto wengi wanapofanyiwa ukatili huo wazazi wao wanashindwa kuwagundua kwasababu ya kutokuwa na muda wa kuzungumza nao.

Wengi wa wazazi wanafikiria namna ya kuingiza pesa ili kumudu kuendesha maisha ikiwamo kusomesha watoto bila kufikiri kuwa ana wajibu wa kuzungumza na mtoto wake kujua maendeleo yake na changamoto anazokutana nazo.

Mzazi anapokuja kugundua kuwa mtoto wake anapitia changamoto ikiwamo ya ukatili anakuwa ameshachelewa na mtoto amesha athirika.

Matukio mengine yanasikitisha kwasababu wanaofanya ukatili kwa watoto ni wazazi wenyewe kwa madai ya kufanya kosa la kudokoa mboga, kuiba pesa na mengine ambayo kama mzazi angekaa naye na kumuonya ukatili kama huo asingeweza kuufanya.

Ukatili ulioshamiri hivi sasa ni watoto hasa wa kiume kuingiliwa kinyume na maumbile. Hali hii inasikitisha na mzazi anaposikia mtoto wake anafanyiwa kitendo hicho uchungu wake hauwezi kuelezeka.

Lakini, cha kushangaza wazazi wengine ndio wanaowafanyia watoto wao vitendo hivyo pengine kwa imani za kishirikina ili apate utajiri na wengine huwezi kuelewa kama ni ugonjwa wa akili au la. Baadhi ya wanaofanya ukatili wa aina hiyo hufikia hatua ya kuwatoa uhai watoto hao kama ilivyotokea huko wilayani Temeke.

Inasikitisha watoto wasio na hatia kutolewa uhai na kuzimwa ndoto zao. Pengine wangekuja kuwa viongozi wa kusaidia taifa, lakini wamezimwa bila huruma.

Kuna tukio pia lililoripotiwa huko mkoani Lindi ambako inadaiwa mwalimu kumshawishi wanafunzi wake amwingilie kinyume cha maumbile.

Hili nalo ni tatizo lingine, walimu wanaotegemewa kufundisha maadili mema wanafunzi wao, ndio wanaowafundisha njia mbaya. Mwanafunzi kama huyo anayefundishwa vitendo hivyo matokeo yake atazoea na kuwageukia wanafunzi wenzake.

Kuna umuhimu mkubwa wa wazazi kurudi kwenye majukumu yao ya ulezi kwa kufuatilia nyendo za watoto wao kila siku na kuongea naoi li kudhibiti vitendo hivyo vya kikatili.

Wazazi wakumbuke kuwa wao ndio waliowaleta watoto hao duniani na jukumu la kwanza la ulezi ni lao, si la mwalimu au jiriani.

Mtoto pia anapoonekana kubadilika tabia na kuanza kujitenga, lazima afuatiliwe ili kujua tatizo linalomkabili.

Upo umuhimu wa shule kuzingitia mafunzo ya elimu ya dini ili watoto waweze kuwa na maadili mema na kumwogopa Mungu. Mmomonyoko wa maadili unachangiwa pia na watu kutokuwa na hofu ya Mungu na kufanya vitendo vya ovyo.

Hivi sasa ni bora ukutane na mnyama usiku anaweza akakimbia, lakini binadamu atakufuata na kukuzuru.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi, watumishi waache tabia ya kiburi na majivuno

**AKIWA** kwenye ziara ya kusikiliza kero za wananchi huko Wete, mkoa wa Kaskazini Pemba, Mbunge wa Kojani, Hamad Hassan Chande aliwataka viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), wilayani humo kutokuwa na majivuno wala kiburi wanapokuwa madarakani, akisema huo si utaratibu wa chama.

Akiwa Kigongoni, wilayani Wete, aliwataka viongozi wa chama hicho kuwa wanyenyekevu na ushirikiano kwa vijana ambao wameonyesha nia ya kujiunga.

Hili lilizungumzwa na Chande ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri ya CCM Taifa, haliwezi kupita bila kupongezwa.

Ingawa alikuwa akiwazungumzia viongozi wa Wete, lakini ukweli ni kwamba hili suala ni mtambuka, lipo kwa hata viongozi wengine ambao wameteuliwa na Rais, wabunge, na hata watumishi wa umma.

Baadhi yao wamekuwa na tabia ya majivuno na kiburi kwa wananchi ambao ndiyo wanawafanya wanalipwa mishahara kutokana na kodi zao.

Waswahili wanasema kiburi si maungwana, lakini jambo hili limekuwa sugu hasa wananchi wanapokwenda sehemu ambazo wanatakiwa kupata huduma.

Hapo ndipo utakapoona rangi halisi ya mtu ambayo inawezekana kuwa hukumtarajia kufanya hivyo.

Mara nyingi binadamu anakuwa mtulivu anapokuwa hana kitu, lakini akipata madaraka na pesa anabadilika tabia.

Ndiyo maana wapo wanaosema ukitaka kujua tabia halisi ya mtu, apate cheo, pesa au vyote viwili.

Ukiona hajabadilika, basi shukuru Mumgu, ujue huyo mtu hiyo ndiyo tabia yake halisi, hawezi kubadilishwa na chochote kile.

Sasa kuna wale ambao hubadilika wanapokuwa na mamlaka, au ukubwa sehemu fulani, basi inakuwa tatizo.

Hawa unaweza kuwakuta sehemu ambazo zina uhitaji wa kijamii kama kwenye ofisi za umma, zahanati, hospitali, mahakamani na sehemu zingina zinazofanana na hizo.

Hapa tunaona wanaowajibu wananchi maneno yasiyofaa, kuwabeza, wakuwadharau, kuwatisha hata kukataa kuwapa huduma.

Wapo hata baadhi ya viongozi ambao wanawatimua watu wanaokwenda kupeleka shida zao ofisini.

Lakini shughuli inaanza tu pale wanapokutana na wasaidizi wao, ambapo dharau zitaanza, maswali ya kukera yataulizwa, lakini kwa sababu mtu ana shida ataendelea kuvumilia.

Hata hivyo, baadhi yao wanajikuta wakishindwa kukutana na kiongozi kwa sababu ya kujifanya 'mungu mtu', bila kutafakari kuwa watu hao ambao hataki kukutana nao ndiyo waliomfanya kuwa hapo, na hiyo ndiyo moja ya kazi yake.

Hicho ki kiburi na dharau. Ukikutana na wananchi wengi hasa wa hali ya chini, anaweza kukusimulia angalau kisa kimoja alichofanyiwa alipokwenda kutafuta huduma.

Kwa maoni yangu nawakumbusha kuwa cheo ni dhamana, na pesa ni maua, huchanua na kunyauka.

Kuwa na wadhifa, ni kama mtu anayepanda au kwenda juu, ni lazima itafika wakati atashuka chini.

Mimi nadhani wakati mtu akiwa na wadhifa, ndiyo muda wa kutengeneza marafiki wa kweli, ili akitokea aliyekupa akichukua cheo chake na kumpa mwingine, wale wa chini waweze kukupokea ili uishi kwa amani na jamii.

Kwa sababu mimi nafahamu kuwa watu wetu walio ndani ya jamii pamoja na umasikini wao na kutokuwa na uwezo wa kufanya chochote, lakini hawasahau kitu na nguvu yao pekee wanayobaki nayo kwa watu wa aina hiyo ni kuwatenga wanapokuwa hawana tena madaraka kutokana na kuwadharau na kuwatendea vibaya walipokuwa juu.

Muhimu ni kila mmoja afanye kazi zake ipasavyo bila ya kuwanyanyapaa watu kwa kiburi na majivuno, kwa sababu kuna maisha baada ya cheo.

Wakikutenga utaishi na 'stresi' mara mbili, kutokuwa na cheo na kutengwa, inaweza kusababisha hata kufupisha maisha.

# Mwenezi CCM abebeshwa kero barabara, atakiwa kufuatilia ahadi

**Na Kulwa Mzee**

KATIBU Mwenezi wa CCM Wilaya ya Ilala, Mwinyimkuu Sangaraza, amebebeshwa mzigo wa lawama kwa barabara mbovu za Kivule na kutakiwa afuatilie ahadi ambazo hazijatekelezwa hadi sasa.

Sangaraza amekutana na kero hizo jana alipokuwa mgeni rasmi katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kivule, Amos Hangaya, akizungumzia utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Kata ya Kivule, Jimbo la Ukonga.

"Barabara ni kero kubwa, tuliahidiwa zitatengenezwa Aprili, mwaka huu haikuwa, tukaambiwa Julai na sasa Julai imefika tunakubebesha mzigo huu Mwenezi, kero ya barabara imekuwa ya muda mrefu.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa fedha, tunakuachia hili ulibebe, utufikishie kwa wahusika, barabara zitengenezwe haraka, ndoa nyingi zinaingia kwenye migogoro chanzo ni shida ya usafiri inayotokana na ubovu wa barabara," alisema Hangaya.

Akijibu, Katibu Mwenezi Sangaraza alisema amelibeba tatizo la barabara za Kivule atalifikisha lifanyiwe kazi.

"Viongozi wa manispaa wanaelewa tatizo la barabara za Kivule, wilayani kuna ushirikiano mkubwa kati ya viongozi wa chama na serikali.

"Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala tunao pale, nitalifikisha hili jambo kwa viongozi wa manispaa, kero ya barabara iliyopo Kata ya Kivule itaondoka siku sio nyingi," alisema Sangaraza.

Akizungumzia kero hiyo, Diwani wa Kata ya Kivule, Nyansika Getama, alisema juzi alikuwa kwenye kikao cha barabara manispaa na kwamba itajengwa kwa kiwango cha zege hadi Msongola.

Alitaja barabara zingine zilizojadiliwa kujengwa ni Njiapanda Sokoine hadi Magole, Shule ya Mshikamano hadi Hospitali ya Wilaya Kivule, Bombambili hadi kwa Msumi na Kwamkoremba.

Alisema magreda matatu ya manispaa tayari yamefufuliwa na kuanzia wiki ijayo yatakuwa barabarani kwa ajili ya kazi ya barabara.

"Nawaomba wananchi tujitahidi tusizibe barabara, barabara ndio kila kitu zitajengwa pamoja na vivuko, nawaasa muwe wavumilivu," alisema Nyansika.

Akizungumzia changamoto za wanafunzi katika Kata ya Kivule, Hangaya alisema wamefanikiwa kupunguza gharama za michango shuleni kutoka Sh. 2,100 hadi 1,200 na watoto wanapata chakula wanapokuwa shule.

"Tumefanikiwa kusimamia watoto 80 waliokuwa wanaingia 'chaka' yaani watoro na wameweza kufaulu kuingia sekondari.

"Wanafunzi hao wakiwamo wa shule ya msingi na sekondari waliwekewa utaratibu, wakitoka shule wanapitia Kituo cha Polisi Kivule kutia saini daftari kuthibitisha wametoka shule huku wakionyesha daftari la mwalimu lililosainiwa kuonyesha walihudhuria darasani.

"Watoto hao wamefaulu sasa hivi wako sekondari na wengine walimaliza kidato cha nne wako kidato cha tano," alisema Hangaya.

Alisema changamoto za madarasa na madawati hakuna tena katika shule zilizopo kwenye kata hiyo.

Aidha, wamefanikiwa kuondoa migogoro ya makanisa na misikiti ilivyokuwa kipindi cha nyuma na sasa kakuna katika nyumba hizo za ibada.




Mgombea urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili wa Mahakama Kuu, Sweetbert Nkuba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu ilani yake kuelekea Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 24 mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# H'shauri za Pwani zachanga mil. 19/- kuokoa vifo mjamzito, mtoto mchanga

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ZAIDI ya Sh. milioni 19 zimechangwa kutoka katika halmashauri tisa za Mkoa wa Pwani ili kufanikisha mfumo wa usafirishaji wa dharura wenye lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga (M-MAMA), kufanya kazi bila vikwazo.

Fedha hizo za mapato ya ndani ni kwaajili ya kuwezesha mfumo huo kutekelezeka kuanzia ngazi ya jamii ambako mjamzito na mtoto mchanga mwenye changamoto atasafirishwa kufikishwa kwenye kituo kupitia madereva waliosajiliwa.

Hayo yamebainishwa jana mjini Kibaha na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, David Vuo, alipokuwa akizungumza na maofisa habari na waelimisha umma kuhusu mfumo wa M-MAMA ambao unatekelezwa nchini, ukiwamo Mkoa wa Pwani.

Vuo alisema hadi Julai 9, mwaka huu, rufani za dharura 2,207 zimesafirishwa kwenye mfumo na safari zilizoratibiwa na magari ya kubeba wagonjwa zimefikia 2,084 sawa na asilimia 93.06 na kupitia madereva ngazi ya jamii ni 14 sawa na asilimia 6.38.

Kwa mujibu wa Kaimu Mganga Mkuu, tangu kuanzishwa mfumo huo umepunguza vifo vya watoto wachanga kutoka 358 kwa mwaka 2023 hadi 178 mwaka huu na wajawazito 37 hadi 12 kwa kipindi hicho.

Alisema awali, usafirishaji wa dharura kwa mjamzito na mtoto mchanga ulikuwa kituo kwa kituo na sasa unaenda kupatikana ngazi ya kijiji, wenye changamoto watakapopiga simu dereva aliyesajiliwa atawafikia walipo na kuwafikisha katika kituo cha afya.

Mratibu wa M-MAMA Mkoa wa Pwani, Alfred Ngowi, alisema waelimishaji wa M-MAMA ngazi ya jamii sasa wanakwenda kufanya kazi kufika ngazi ya kijiji na watasaidia kuwainua wajawazito wenye changamoto pamoja na watoto wachanga waweze kupata huduma kwa haraka.

Mmoja wa waratibu wa M-MAMA kutoka Halmashauri ya Chalinze, Gabriela Mtwale, alisema mafunzo wanayopatiwa yatawaimarisha zaidi katika kazi yao ya kufikia jamii na kuielimisha kuhusu mfumo huo.

Gabriela alisema, awali mjamzito alikuwa anakumbwa na changamoto iliyosababishwa na kukosa usafiri wa kumfikisha kituoni kwa haraka tofauti na sasa atapiga simu akiwa nyumbani na atafuatwa na kuwahishwa kituoni.

Alisema utaratibu huo pia utafanyika kwa watoto wachanga na endapo watazingatia elimu hiyo itasaidia kuondoa vifo vinavyochangiwa na baadhi ya familia kukosa fedha kwa ajili ya kumuwahisha hospitali mjamzito au mtoto mchanga na huduma hiyo kwa sasa itatolewa na serikali.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# POSITION ANNOUNCEMENT
# ASSISTANT SCIENTIST
# IITA-TZ-2024 - IRRI-009 -NRS- BAGAMOYO

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Assistant Scientist.**

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium.

The Assistant Scientist under the Inclusive Markets and Value Chain (IMVC) Unit will be part of the unit's market intelligence covering Sub-Saharan Africa. The successful applicant will assist and support in designing and conducting research studies related to market intelligence, consumer and farmer behaviour, and product concept design and testing. Furthermore, the incumbent will support the team in implementing mixed method approaches to generate and validate market and behavioural intelligence to inform the design of product profiles while engaging with multiple stakeholders across CGIAR's Genetic Innovation Stakeholder Network. Additionally, the incumbent will assist the IMVC and the Transformative Policies and Investments Unit in implementing monitoring and evaluation activities across different projects.

The candidate will also assist in the improvement and development of research tools, data collection, analysis and interpretation of results, scientific publication in international peer-reviewed journals and overall dissemination efforts through reports, policy briefs, and presentations in national/international workshops and conferences

**Duty Station:** The position will be based in Bagamoyo.

**Responsibilities**

**1.1. Purpose**

- Support in identifying stakeholders' current and future drivers of demand for crops, seeds and traits, and variation of demand according to gender, age and social groups, farmer types, agro-industry production requirements as well as consumer preferences
- Contribute to describing prioritized product market segments through reviewing and synthesizing sets of maps, articles and reports that describe prioritized market segments, to enable market intelligence for the design of gender-intentional product profiles
- Support in characterizing varietal demand to enable market intelligence for the design of seed system strategies. This will be through reviewing regional and crop-specific bulletins, reports and articles on demand and supply for seed, among other methodologies
- Assist with the implementation of mixed-method social-science research
- Assist with the implementation of monitoring and evaluation activities
- Assist in consolidating, evaluating, verifying and analyzing data related to research studies.

**1.2 Engagement**

- Contribute to collaborative engagement on methods and tool design to ensure comparability of results across crops and regions, not only in Africa but also globally
- Contribute to the strengthening the technical capacity of One CGIAR and its partners to use advanced tools and methods that convert global and regional challenges into regional impact opportunities for Genetic Innovation
- Support in initiating institutional change process by building regional, transdisciplinary CGIAR-NARES-SME teams
- Organize regular meetings with partners and stakeholders to discuss, streamline and implement activities
- Support in the development and communication of guidelines to internal and external stakeholders to bolster a collaborative implementation of project and programme activities

**1.3 Delivery**

- Identify resource persons and ensure the logistics are appropriate for defined purposes and engagement tasks
- Support in the verification of suggested methodologies and activities as well as draft training materials using both primary and secondary data sources
- Establish and maintain strong communication with NARES and CGIAR partners
- Implement activities geared towards a common framework by the identification and description of product market segments, gender-disaggregated assessment of needs and preferences for traits as well as prioritization of product market segments across regions and crops for scalability
- Provide inputs into activities geared to inform prioritization via foresight market intelligence analyses
- Support project and programme activities for monitoring and evaluation

Perform any other relevant duties as assigned by supervisor from time to time

**Qualifications and experience**

- MSc in social sciences preferred disciplines include psychology, sociology, anthropology, development studies, agricultural extension, environmental geography, or any other discipline that provides suitable advanced knowledge in social science with at least 3 years' experience.

**Skills and knowledge**

**1.1 mandatory**

- Has proven technical proficiency in using qualitative and quantitative social science methods
- Has strong oral and written communication skills
- Has strong analytical skill
- Has good presentation skills
- Has excellent computer skills
- Is able to work independently with very minimal supervision

**1.2 Preferred**

- Experience in qualitative research methods, experience in identifying, setting up, and maintaining multi-stakeholder partnerships, Experience with qualitative impact assessment.

**Work Condition and environment**

May require occasional travels to other countries where IRRI operates.

**General information:**

**General information:**

The duration of the contract for all the four positions is two years renewable subject to performance and availability of funds. These are nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

The application pack should include an application letter, copies of certificates, and a curriculum vitae which contains a telephone number, email address, and contact details of two referees. Applications should be sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org** and addressed to:

**The Country Representative, IITA-Tanzania,**
**Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road,**
**Mikocheni Industrial Area,**
**Dar es Salaam, Tanzania**

Applicants are requested to include the **reference number for the position** (as indicated on the heading of the announcement) in the subject of their application letter, as well as in the subject of their email. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date for applications: Thursday 25th July 2024.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.



# Wanaochangishana ‘buku’ wamwangukia Kairuki

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKAZI wa Kata ya Kilema Kaskazini Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, Angelah Kairuki kufungua barabara ya Kilema ili kukuza utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) na uchumi wa wananchi.

Wameiomba serikali kutoitumia kama barabara ya dharura badala yake itumike kama barabara maalumu ya kupandisha watalii kwenda kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro na kuchochea uchumi wa eneo hilo linalopakana na hifadhi hiyo.

Mratibu wa mradi wa ujenzi huo wa barabara za vijiji vya Makami Chini na Makami Juu, Wolter Nguma, alitoa ombi hilo juzi wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara 11 za kata hiyo na Kampuni ya kizawa ya Milioni Engineering General Supply.

Wakazi hao wamechangishana kuanzia Sh.1,000 kila mmoja kupitia Kikundi cha Maendeleo ya Kata hiyo cha ‘WANAMAKAMI’ kwa ajili ya kuzijenga barabara zao.

“Ndio maana tunazidi kupigania barabara hii ya Kilema iweze kufunguliwa kwa ajili ya shughuli za utalii. Maana yake ni kwamba kama barabara ya TANAPA ikijengwa vizuri, matokeo yake vijiji vingine vitakuwa na uwezo sasa wa kuanza kujengwa hoteli na vitu vingine vya namna hiyo.

...Ukiangalia bado tunahitaji teknolojia kwenye masuala ya kilimo, migomba ambayo tunayoitumia sasa hivi bado ni ya kizamani, ukiangalia miti ya kahawa iliyoko bado ni ya zamani, kwa hiyo bado tunahitaji wale wataalamu wa kilimo kuja katika maeneo haya na kuweza kuleta mabadiliko.

Alisema wemeanza kama kikundi, lakini wanaamini serikali ikishirikiana nao, wakazi hao wataondokana na umasikini wa kipato.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Makami Juu, Happynes Samweli, alisema kama serikali itaridhia barabara hiyo kufunguliwa kwa ajili ya shughuli za utalii, itapunguza umasikini wa kipato kwa wakazi wa kijiji hicho.

Kata ya Kilema Kaskazini, pamoja na mambo mengine haina Kituo cha Afya wala Kituo cha Polisi.

# Wizara yaagiza taarifa za wateja zilindwe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imewaagiza maofisa wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOS) kutoka Umoja wa Benki Tanzania (TBA) na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano nchini (TAMNOA) kulinda taarifa binafsi za wateja wao.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mohammed Khamisi Abdula, alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Maofisa hao wanapatiwa mafunzo hayo kwa ajili ya kutimiza lengo la ukusanyaji na uchakataji wa taarifa kutoka taasisi za benki na kampuni za simu nchini.

“Mafunzo haya ni hatua muhimu kuelekea kulinda faragha za watu, katika zama hizi za uchumi wa kidijitali. Hakikisheni mnafanya kazi kwa umakini ili wateja wenu muwalinde kwenye taarifa zao,” alisema Abdula.

Alisema katika dunia ya sasa ambayo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yameendelea kukua, taarifa binafsi zimekuwa bidhaa muhimu na nyeti kutokana na matumizi yake katika biashara, afya, elimu na shughuli mbalimbali za serikali.

“Ulinzi wa taarifa binafsi hauhusu tu kufuata sheria, bali ni suala la maadili na uaminifu. Watanzania wanategemea taarifa zao zitatunzwa kwa usalama na zinatumiwa kwa uangalifu mkubwa kama Katiba yetu Ibara ya 16 inavyoelekeza.

“Sote ni mashuhuda kuwa Serikali imeweka mfumo wa Kisheria kwa kutunga Sheria Mahususi ‘Sheria ya ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022 na kanuni zake, lakini pia kuweka

mfumo wa kitaasisi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo,” alisema.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu yao ya kitaasisi, wamekua wakikusanya, kuchakata na kusafirisha taarifa binafsi za watu, hivyo ni muhimu kuzingatia misingi iliyopo kwenye Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Kulingana na Abdulah, washiriki hao watapata fursa ya kujifunza mambo kadhaa ya ulinzi wa taarifa binafsi kuhusu sheria na kanuni za Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ikiwa ni pamoja na Sheria ya ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022 na kanuni zake.

Vilevile, mbinu na mikakati bora ya kulinda taarifa binafsi dhidi ya udukuzi, wizi, na matumizi mabaya na kuelewa jinsi ya kutambua na kusimamia hatari zinazohusiana na usalama wa taarifa binafsi.

“Mafunzo haya yatawaongezea ujuzi wa kubaini na kupunguza hatari zinazohusiana na matumizi yasiyo sahihi ya taarifa binafsi za wateja wao, lakini mtaweza kubaini maeneo yenye hatari zaidi katika mifumo yenu na kuchukua hatua stahiki,” alisema.

Alizihimiza taasisi nyingine kukamilisha usajili baada ya utekelezaji wa sheria kuanza.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa taarifa binafsi, Balozi Adadi Rajabu, alisema mafunzo hayo ni hatua ya kwanza kuhakikisha wanajenga uwezo wa kutosha katika sekta hizo muhimu ambazo zinahusika moja kwa moja na taarifa za watu.

Adad, alisema makampuni ambayo yanahifadhi na kushughulikia taarifa nyeti za wateja, elimu hiyo ni muhimu zaidi.

Alisema kwa kuwaelimisha maofisa wa ulinzi wa taarifa binafsi kuhusu mbinu bora za kulinda taarifa hizo, watasaidia kupunguza hatari ya udanganyifu, wizi wa utambulisho na uvunjifu wa faragha. Alitoa wito kwa sekta zote husika kushirikiana na tume hiyo kuhakikisha viwango vya usalama wa taarifa vinazingatiwa na kujenga mazingira salama kwa taarifa za watu.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. 14442 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

FARIDA ABDALLAH MBARAKA.........................................ACCUSED PERSON

To:
Farida Abdallah Mbaraka
Plot No. 212, Block U, Mwasele Area
Shinyanga

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 25th day of July, 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ....4TH.... day of ....July.... 2024

DISTRICT COURT, SHINYANGA — TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE P.O. Box 29 - SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name. ..........................................
Signature..........................................
Qualification/Relationship
Date..........................................

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF SHINYANGA
*(AT SHINYANGA)*

CRIMINAL CASE NO. 14441 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

FAHIM SAID ABDALLAH.........................................ACCUSED PERSON

To:
Fahim Said Abdallah
Plot No. 215, Block U, Mwasele Area
Shinyanga

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 25th day of July, 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ....4TH.... day of ....July.... 2024

DISTRICT COURT, SHINYANGA — TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE P.O.Box 29 - SHINYANGA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name..........................................
Signature..........................................
Qualification/Relationship
Date..........................................





# Wanafunzi 600 wajisaidia choo cha nyasi, vichakani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ZAIDI ya wanafunzi 600 wa Shule ya Msingi Nzonza wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya milipuko kwa kujisaidia kwenye tundu moja la choo cha nyasi na wengine vichakani baada ya walivyokuwa wakitumia kufungwa baada ya kutitia.

Hayo yalibainika juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro uliofanyika kwa ajili ya kusikiliza kero za wakazi wa Kata ya Salawe kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi.

"Wanafunzi 624, wanatumia choo kimoja tu baada ya vyoo vilivyokuwepo kutitia na kufungwa ili visitumike tena, wanakijiji tukaona tuchimbe tundu moja la choo na kuzungushia nyasi ili litumike, lakini wanafunzi wengi hujisaidia vichakani na bado hakuna utaratibu kukabili hali hiyo," alisema

Akijibu kero hiyo, Mtatiro aliiagiza Halmashauri ya Wilaya hiyo kufanya tathmini ya vyoo kwa shule zake zote na ujenzi kufanyika haraka ili kunusuru afya za wanafunzi dhidi ya magonjwa hayo.

Kuhusu kukithiri kwa michango kwa wananchi kwa kata nzima na kutosomewa mapato na matumizi ya fedha, Mtatiro alipiga marufuku uchangishaji holela na kuamuru ifanyike baada ya ofisi yake kuidhinisha.

Akijibu malalamiko ya ukosefu wa umeme ikiwemo kwenye taasisi za serikali na ujenzi wa zahanati kutokamilika, ukiritimba utoaji mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu, aliahidi kufuatilia ili yamalizwe mapema iwezekanavyo.

Kuhusu kukithiri kwa vitendo vya ujambazi watoto kuliwa na fisi na kituo cha afya Salawe kutofanya kazi, aliahidi kuyapatia ufumbuzi.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wakazi wa Salawe na kuzitafutia ufumbuzi, wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kaya 2,000 zaondolewa TASAF

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

KAYA 2,000 kati ya 5,349 wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) wilayani hapa Mkoa wa Mwanza zimeondolewa katika mpango huo baada ya kufuzu kujiimarisha kiuchumi.

Hayo yalibainishwa mapema wiki hii na Mratibu wa Mpango huo, Leonard Robert wakati akizungumza na wahitimu hao na wanufaika wengine wa mpango huo.

Kwa mujibu wa Robert, mwaka 2023 kupitia TASAF, walifanya tathmini kwa walengwa na kubaini kaya zilizoimarika kiuchumi.

Alisema kaya hizo zilibainika kukidhi vigezo vya kuondolewa huku 3,349 zikiendelea kupokea malipo kutoka kwenye mpango huo.

"Kuondolewa katika mpango haimaanishi vile vikundi vyetu vya TASAF vimekufa, kaya zilizoimarika zinaweza kuendelea kukutana na zikatumia vikundi hivyo kupanga mipango ya kujiendeleza kiuchumi hata kunufaika na mikopo ya halmashauri kupitia mapato yake ya ndani," alisema Robert.

Alisema hatua ya kubaini kaya zilizoimarika kiuchumi ni endelevu na zitakuwa zikiondolewa kadri ya zinavyofuzu katika mpango huo.

Mwezeshaji wa TASAF Manispaa ya Ilemela, Mkama Costantine, alishauri kaya zilizosalia kutumia fedha wanazopewa kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato.

Constatine, alisema kaya hizo zinapaswa kutambua ipo siku zitatoka katika mpango huo na kutumia fursa ya vikundi kukopa katika taasisi za fedha na halmashauri kujiimarisha kiuchumi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ustawi Kata ya Buzuruga, Bahati Kabadi alizipongeza kaya zilizotoka katika mpango huo kwa kutumia vizuri fedha walizopata kwa uzalishaji mali na kujiimarisha kiuchumi huku akisisitiza zilizosalia kuiga mfano huo.

# Ndejembi aagiza wenye ualbino walindwe

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Deogratias Ndejembi amewaagiza wakuu wa mikoa,wilaya na wakurugenzi wa halmashauri nchini kuwalinda watu wenye ulemavu, wakiwemo albino.

Ndejembi, alisema viongozi hao wanatakiwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria namba 9 ya mwaka 2010 ya kuwalinda watu hao katika maeneo yao.

Alikuwa akizindua kampeni ya kupinga ukatili dhidi ya wenye ualbino juzi wilayani Muleba, ikiwa ni mwezi mmoja tangu lilipotokea tukio la kuibwa mtoto aliyekuwa na ualbino na kuokotwa akiwa amekufa na kuondolewa baadhi ya viungo vya mwili wake.

Alisisitiza kuwa utekelezaji wa sheria hiyo uendane na usajili na utambuzi wa wenye ualbino katika mitaa na vijiji na kwamba jukumu hilo linatakiwa kutekelezwa na watendaji wa maeneo hayo kwa lengo la kulilinda kundi hilo.

Ndejembi, alisema uandikishaji huo kisheria unaendana na sheria za kimataifa zinazosisitiza ulinzi kwa watu wenye ulemavu duniani.

Alisema Serikali imefanya uimarishaji haki na ustawi wa wenye ulemavu, kutoa mafuta ya ngozi kwa wenye ualbino kwa kuikabidhi Wizara ya Afya Juni 13 mwaka huu ikiwa ni siku ya kimataifa ya kukuza uelewa kwa kundi hilo.

Alisema Serikali iliweka kiasi cha Sh. bilioni moja ikiwamo ruzuku ya uendeshaji wa vyama wa wenye ualbino nchini (TAS).

Kaimu Katibu wa Chama cha wenye ualbino nchini, Alfred Kapole, alisema ulinzi na elimu ni jambo la kila mmoja katika jamii kwa kuhakikisha kuwa upo usalama wa uhakika kwa wengine.

Alisema kuwa ulinzi na usalaa wa raia upo mikononi mwa Jeshi la Polisi na ndani ya jamii ili kutokomeza vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya walemavu.

Alisema inatakiwa elimu kutolewa kwa jamii ili ifahamu aliye na ualbino ni sawa na asiyekuwa nao. "Nizidi kuomba utetezi kwa kundi hili kwani wanaokuwa wakifanya ukatili wanatokea ndani ya jamii wakidhani kuwaondolea viungo vya mwili watapata mafanikio," alisema.

Mkuu wa Mkoa huo, Fatma Mwasa, alisema suala la ulinzi kwa wenye ualbino linawagusa pia waganga wa jadi na viongozi wa dini.

Mwasa, alisema makundi hayo mawili yana nguvu kubwa za ushawishi wenye kuelimisha jamii juu ya ulinzi wa watu hao ndani ya jamii zetu ili waweze kuishi.

Alisema Kagera una wenye ualbino 275, kati ya hao, jinsia ya kiume 142 na kike ni 133.



Ukurasa 12

WACHIMBAJI WADOGO WA SONGWE...
Ahadi waliyopewa na Samia akiwa Makamu, watamba matunda wanayafaidi akiwa Rais




Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA JULAI 12, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## MAMA SAMIA LEGAL AID...

# Kampeni ya Rais inayowatumikia wananchi msaada sheria 'bei bure', ikiwafikia 490,000

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPENI ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyopewa jina la 'Mama Samia Legal Aid Campaign', iliyozinduliwa mwaka jana imeanza kuleta matumaini ya utatuzi wa migogoro sambamba na kufanyika kuwa shule ya elimu ya masuala ya kisheria kwa wananchi.

Kampeni hii ambayo inatarajiwa kufanyika kwa miaka mitatu mpaka mwaka 2026 Februari katika pande zote mbili za Muungano, tayari imewafikia wananchi 490,000 katika mikoa saba ya Dodoma,Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara, Njombe na Ruvuma.

Miongoni mwa maeneo inayogusa ni pamoja na katika kutoa elimu ya kisheria kwa wananchi hususani katika masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala, na masuala yahusuyo haki za binadamu kwa ujumla.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi akizungumza na Nipashe katika maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaama(DITF) yanayoendelea barabara ya Kilwa wilayani Temeke ambayo huduma kupitia kampeni hiyo inatolewa, anasema Wizara imeona kuna umuhimu wa kupeleka huduma kwenye maonesho



Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, akimhudumia mwananchi aliyefika katika banda la Msaada wa Kisheria la Mama Samia, maarufu kama Mama Samia Legal Aid Campaign, kwenye Maonyesho ya Sabasaba, Barabara ya Kilwa Temeke. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

hayo ili kuwasaidia wananchi.

"Kwa hiyo tuko hapa kuungana na wadau wengine katika kuhakikisha mwananchi hakosi huduma yoyote ya kisheria akiwa katika viwanja hivi vya sabasaba, kwa hiyo kama kuna mtu ana jambo lake linamtatiza na anataka litatuliwe kisheria atumie fursa hii ya maonesho,tuko mpaka mwisho kuhakikisha tunawafikia wananchi wengi zaidi,"anaesema Ester.

Anasema mfano kesi ambazo wakili anaweza kumsaidia mwananchi baada ya kufika katika kampeni hiyo ya kitaifa ni pamoja na hati za kufungua mashauri mahakamani iwe ni kufungua kuomba usimamizi wa mirathi, masuala ya madai,matunzo ya watoto, kuasili watoto na masuala mengine ya kisheria ambayo nyaraka zake zinapelekwa mahakamani.

Huduma nyingine anasema ipo mikataba ambayo mtu anaweza kusaidiwa kuandika pamoja na huduma nyingine ambazo mwananchi wa kawaida hawezi kwenda kuzipata kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumlipa wakili.

Ester anasema tangu yalipoanza Maonyesho ya Sabasaba, Juni 28 mwaka huu, mwitikio wa wanachi wanaojitokeza kuomba kutatuliwa migogoro yao inayohitaji msaada wa sheria ni mkubwa.

Kwa mujibu wa Ester, utekelezaji wa kampeni hiyo unafanyika kwa kushirikiana na wizara na taasisi za serikali, asasi za kiraia, wanazuoni na wadau wa maendeleo.

Ester anasema lengo kuu la kampeni ni kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini.

Pia, anasema katika kufikia lengo hilo, kampeni inaongeza uelewa wa kisheria na haki za binadamu kwa jamii hususani haki za wanawake na watoto, inatoa huduma ya ushauri wa kisheria na unasihi kwa waathirika na manusura wa ukatili wa kijinsia,kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya sheria, masuala ya haki na wajibu na misingi ya utawala bora.

"Matokeo ya muda mrefu wa kampeni hii ni kuchangia katika kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wasiojiweza, hususani wanawake, watoto na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi.

"Vilevile, itachangia kuimarisha amani na utulivu, kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na kuleta utengamano wa kisiasa hapa nchini,"anasema Ester.

Kwamba matokeo ya kati ni kuimarika kwa mfumo wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi za serikali kuu hadi serikali za mitaa.

Na matokeo ya muda mfupi anasema ni kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotoa taarifa

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

### WACHIMBAJI WADOGO WA SONGWE...

# Ahadi waliyopewa na Samia akiwa Makamu, watamba matunda wanayafaidi sasa Rais

**Na Ibrahim Yassin, SONGWE**

SONGWE ni mkoa unaozalisha madini, ikiwamo dhahabu, yenye mchango mkubwa kutatua changamoto ya ajira kwa vijana na ukuaji uchumi wilayani Songwe, mkoa hadi taifa.

Akiwa Makamu wa Rais katika serikali Awamu ya Tano, Dk. Samia Suluhu Hasan, alifika wilayani Songwe na akafanya mazungumzo na wachimbaji wadogo, kupitia umoja wao akipokea kero zao mbalimbali.

Mojawapo walioitaja ni ukosefu wa maeneo ya kuchimba madini, kwani kila eneo walilotaka kuchimba waliambiwa 'ni la mtu', hivyo wakalalamika kuwa maisha magumu, baadhi yao wakiingia kwenye uhalifu na wizi.

Kuna vikao vilifanyika vya namna ya kuwasaidia vijana hao tangu zama hizo za Serikali Awamu ya Tano, hatimaye sasa miaka mitatu ya Rais Dk.Samia, vijana wamefanikiwa kukata kiu yao wakipatiwa vitalu 19 kati ya 35 walivyoomba na tayari wameanza kuchimba madini.

Katibu wa Chama cha Wachimbaji Wadogo Mkoani Songwe (SOREFA), Elias Pangani, anasema upatikanaji vitalu umeibua ajira kwa vijana 12,000, pia ikifuta vitendo vya uhalifu kwa vijana wakihamia kwenye uchimbaji na nafasi.

Anasema kuna changamoto ya kukosa soko la uhakika la kuuza dhahabu, kwani wachimbaji walisafirisha kienyeji kwenda kwenye masoko ya ndani na nchi nje ya nchi, hata ikahatarisha usalama wao na serikali ikikosa takwimu sahihi za madini, pamoja na tozo.

Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ina migodi ya uchimbaji mdogo dhahabu sehemu mbalimbali, akitaja baadhi kuwa migodi ya Shanta, Sunshine, pia mingine ya makaa ya mawe eneo la Magamba.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, akikabidhi hati kwa wachimbaji wa Songwe.**PICHA: IBRAHIM YASSIN.**

**MABADILIKO SOKONI**

Soko la madini mkoani Songwe lipo wilayani Songwe, ambako dhahabu zote zinauzwa kwa bei elekezi na kudhibiti biashara za ujanja, huku ikidhibitiwa na Kamati ya Usalama Wilaya ya Songwe.

Baada ya Mei 8, 2019 lilitoka tangazo la marufuku ya serikali, kutouza madini ya mkoa kwingineko, ikithibitika mahakamani jinai hiyo, adhabu yake ni kutaifishwa mali, kufungwa mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

Maendeleo yake, Pangani anafafanua kuwa mwaka 2020, kila siku kulipatikana kilo tatu za dhahabu zilizouzwa kwa shilingi milioni 270.

Ni soko linalowasaidia wachimbaji wadogo kutambulika na kuzuia utoroshaji madini, haki ikipatikana kwa kila mshiriki anayehusika na sekta ya madini hayo.

Hadi sasa anasema, mkoa wa Songwe una jumla ya leseni 24 za utafiti wa madini; 101 uchimbaji mdogo; tano wachimbaji wa kati na kwa mwezi Machi, mwaka huu, wilaya Songwe ilizalisha kilo za dhahabu 411.1.

Tume ya Madini na Wakala wa Vipimo nchini, walipewa angalizo na uongozi wa mkoa kuhakikisha wanasimamia vifaa na taratibu zitakazotumika kupima madini hayo ili kuepuka malalamiko.

Katibu wa SOREFA mkoani Songwe, anasema uzalishaji madini bila ya masoko ya uhakika ni kazi ngumu, hivyo wazo la uanzishwaji masoko ya madini anampongeza muasisi Hayati Rais Dk.Samia, wakati akiwa Makamu wa Rais, sasa mdai Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wakiahidi ushirikiano.

Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Idris Kikula, anasema wamepokea maagizo ya Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kirusi, kwamba Tume ya Madini itafute masoko na tayari jitihada zinafanyika.

**MAFANIKIO KISEKTA**

Wilaya ya Songwe ni kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, wenyeji ni 229,219 ikiwa na eneo maarufu kata ya Saza, maarufu kwa uchimbaji madini, kukiwapo mgodi wa Shanta.

Madini yaliyoko Songwe yanajumuisha; dhahabu, fedha, huku Ofisi ya Madini Songwe, ilianza ukusanyaji maduhuli ya serikali mnamo Julai Mosi, 2020 ikihudumia wilaya zote za mkoa wa Songwe; Ileje, Momba, Mbozi na Songwe.

Ofisi hiyo ina majukumu ya kupokea na kushughulikia maombi ya leseni, vibali vya madini na baruti; inakagua shughuli mbalimbali za madini; utoaji elimu kwa umma na huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo; kushughulikia kero na malalamiko kwenye maeneo ya madini.

Aina za madini yatokayo mkoani Songwe ni; dhahabu, fedha, shaba, risasi, chuma na madini ya kimkakati (Neodymium na Praseodymium)

Pia, kuna gesi za helium na ukaa; madini ya viwandani (gtranite, Marble, chokaa na chumvi), madini ya vito (fluorite, mica na sodalite), madini ya nishati (makaa ya Mawe) na madini Ujenzi (mawe, mchanga, moramu na kokoto).

Pia, Ripoti ya Mkoa inaonyesha, Songwe ina leseni za uchimbaji mkubwa (SMLs) mbili; utafutaji mkubwa wa madini (PLs) 76; leseni za uchimbaji wa kati (MLs) 28;, na uchimbaji mdogo (PMLs) 1050.

Vilevile ripoti inabainisha Songwe ina vinu vya uchenjuaji dhahabu (Vat Leaching Plants) 203 na Elution Plants 15; leseni za wafanyabiashara wakubwa wa dhahabu 25; na wafanyabiashara wadogo wa dhahabu 140.

Inatajwa utoaji leseni ndogo za uchimbaji madini umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

**UZALISHAJI & UCHIMBAJI MDOGO**

Katika kipindi kuanzia Julai 2020 hadi Mei mwaka huu, inalaezwa Ofisi ya Madini Songwe imeendelea kukusanya maduhuli ya serikali kupitia Soko la Madini Songwe, kutoka kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mkoa inasema katika taraifa yakewezesha Halmashauri ya Wilaya ya Songwe kukusanya ushuru wa huduma shilingi bilioni 1.571.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo mkoani Songwe Emmanuel Kamaka, anasema kwa miaka mitatu mitatu ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita, wamefanikiwa kukuza pato lao.

Anasema, suala la ukosefu wa maeneo ya uchimbaji lilikuwa changamoto sugu na kwamba waliweza kukaa vikao mbalimbali na Rais Dk. Samia wakati akiwa Makamu wa Rais kujadili changamoto zao.

Luganziza Malembo, Ofisa Madini mkoani Songwe, anasema ofisi yake imefanikiwa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini katika kuimarisha ukusanyaji maduhuli ya serikali.

# Kampeni ya Rais inayowatumikia wananchi msaada sheria 'bei bure' ikiwafikia 490,000

Inatoka Uk 11

za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kupungua kwa idadi ya migogoro na matukio yanayotokana na ukosefu wa uelewa wa sheria, kuimarika kwa uwajibikaji na uwezo wa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za msaada wa kisheria.

"Kampeni hii inatoa ushauri au msaada kutoka kwa wataalam wa sheria ili kutatua masuala ya kisheria au kupata ufafanuzi kuhusu haki na wajibu wa mtu pamoja na uwakilishi wa kisheria mahakamani na inafanyika bila malipo," anasema Ester.

"Kampeni hii ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inatoa msaada wa kisheria kwa watu ambao hawawezi kumudu huduma za kisheria kikamilifu au wanaohitaji msaada wa kisheria, ushauri wa kisheria kwa wanahitaji msaada na mwongozo katika eneo hilo ikiwamo masuala ya kifamilia, makazi au ajira."

Ebds "Kampeni inafanya pia kazi ya kumwakilisha mwananchi mahakamani kwa kutoa msaada wa kisheria kwa anayehitaji wakili wa kumwakilisha katika masuala ya kisheria mahakamani na inatoa elimu na ufahamu kuhusu haki za kisheria na jinsi ya kuzitumia."

Ester anasema mbali na hayo, inasimamia usuluhishi wa migogoro kwa kusaidia kuitatua nje ya mahakama kupitia njia za usuluhishi.

Teresia Nyambo mkazi wa Dar es salam anasema anaamini kwamba kampeni hiyo huenda ikawa msaada kwa wanawake wanaotelekezwa na wanaume wakibaki kulea wenyewe watoto.

"Wakina mama wanaachwa wanalea watoto wao peke yao na tunaona baadhi ya watoto wanalandalanda mitaani kutokana na kutelekezwa, tunaomba wanaofanya hivyo wawajibishwe ili iwe funzo kwa wengine.

"Ni bora kama huwezi kumhudumia mtoto usimzalishe, unamzaa halafu unaacha mtaani anateseka hujui anakula nini anaishi vipi halafu baadae akifanikiwa unataka eti akusaidie, watu wawe na huruma na watoto wao.

"Kwahiyo tunashukuru sana ujio wa kampeni hii ya msaada wa kisheria ya mama Samia, tunaamini itasaidia pakubwa, mimi mwenyewe nimekuja hapa nilikuwa na jambo langu lakini hii timu ya wanasheria niliowakuta wamenisaidia na kunipa mwanga mkubwa,"anasema Teresia.

Yunus Milingani naye anasema kupitia kampeni hiyo amepata matumaini ya kutatuliwa mgogoro wake kwenye ardhi.

"Kwa dhati ya moyo wangu, naona jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kwa raia wake, anajitahidi kwa kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao kwa msingi kwamba, haki inainua taifa na dhuluma inaangamiza taifa, nimeshukuru sana kwa hilo,"amesema Milinga.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Nyie TRA njooni kodi nyingine iko huku!




**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008 barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WAKATI nakua na kupata fahamu za kujua kuwapo kwa Mungu, ipo siku wazazi wangu waliniamsha alfajiri na kunivisha nguo ambazo sikuwahi

kuzivaa, zilikuwa mpya; shati na kaptura, tofauti na zamani nikivaa shati refu tu bila kingine chini.

Baada ya kuvishwa nguo hizo nikiwa nimemaliza kuoga, tukala kiporo na kisha kuambiwa tunakwenda mahali nisikokujua na wala nisikotakiwa kuhoji. Safari ilikuwa ndefu kidogo ya mguu, mara nikibebwa na wakati mwingine nikitembea.

Kumbuka sikuwa nimeanza shule, nilikuwa bado kijamaa fulani kidogo hivi nikinyolewa nywele kwa mkasi, kinyozi baba yangu.

Baada ya safari

Kidogo, tukafika jengo fulani refu na kubwa kuliko nyumba tuliyokuwa tukiishi; ya udongo na nyasi.

Tulipoingia ndani, nikasikia nyimbo kila mtu aliyekuwa ndani akiimba.

Tukakaa mahali hivi na wazazi wangu ndipo mtu mmoja akiwa mbele akawa anatuongoza tukisimama na kuimba na mara nyingine kupiga magoti.

Sikuwa najua lolote lililokuwa likiendelea, bali kufuatisha walichofanya wazazi wangu na watu wengine waliojaa mjengoni ambamo baadaye nilikuja kuambiwa linaitwa kanisa na tulikuwa tukienda hapo kila Jumamosi kumwomba Mungu.

Ufahamu na utambuzi ulipozidi kuongezeka, nikataka kumjua huyo niliyekuwa namsikia akitajwa mara zote kwa jina la Mungu. Hatimaye, nikaambiwa ndiye aliyetuumba sote sisi binadamu, lakini siku zote yeye hafiki kanisani bali anaishi mbinguni.

Nikataka kujua mbinguni ni kijiji au mji gani. Nikaambiwa ni huko juu ndiko anakoishi akitufuatilia sisi tulioko huku duniani. Picha ikawa inanijia hasa nilipokuwa nikisikia maneno kama ya aliyeko huko juu mbinguni, ingawa mara nyingi nikitazama juu niliishia kuona mawingu.

Ilinipa matumiani makubwa pale mvua iliponyesha, nikisika wazee wakimshukuru Mungu kwa kuwaletea mvua. Kumbe walikuwa wakishukuru, kwa sababu bila mvua hakuna mazao. Ndipo nikaamini kuwa kumbe huyo Mungu ana uwezo mkubwa.

Nilipoamini hivyo, nikapewa 'madini' mengine tena kuwa Mungu huyo ndiye mmiliki wa jua pia upepo, kwamba akiamua leo jua lisiwake haliwaki au upepo ukatike unakatika.

Alitumiliki sote kama baba alivyomiliki mifugo. Baadaye nikakua na kuelewa kila kitu, nikajua hata kuomba mwenyewe, nikaenda kanisani mwenyewe, nikiambiwa kuna siku Mtoto wa Mungu anayeitwa Yesu naye atakuja kutusalimia na kutuchukua twende naye kumwona Mungu mbinguni.

Furaha iliyoje!

Enzi hizo nakumbuka kuwapo makanisa machache na misikiti, yote yakiwa majengo ya ibada, ya kumwabudia Mungu, kumwomba na kumshukuru kwa

alichotupa hata kama tulilima wenyewe, lakini tukimshukuru kwa kutupa nguvu za kulima.

Nikawa nasikia Kanisa Katoliki, Kanisa la Sabato, Kanisa Anglikana, Kanisa la Pentekoste na Kanisa la Menonaiti na misikiti, basi. Hayo tu, na tukigawanyika hawa wakienda kule Ijumaa, wengine Jumamosi na wengine Jumapili, lakini wote kumwomba Mungu mmoja.

He! Ghafla sijui ukaibuka upepo gani, yakaja mengine kama utitiri, nikiyataja hapa nitamaliza ukurasa! Haya sasa yakawa hayana hata siku maalumu, yanaibukia kokote kuendesha ibada na tena siku yoyote!

Haya sasa yanachangisha fedha za watu kwa jina la Fulani, kwa kiwango kikubwa tofauti na awali tukitoa sadaka kwa hiari, lakini haya ya sasa ni lazima na yakiona mbishi yanakuja na vitisho vya usipotoa hupati baraka za Mungu!

Utalazimika kununua bidhaa zao kwa bei waitakayo wakikwambia ukifanya hivyo ndipo utafanikiwa katika maisha yako.

Watu wanaibiana mali kwenye ndoa wanapelekea ili kupata uzima, watu wanajinyima kula wakiacha kununua chakula cha familia wanawapelekea.

Yametokea nchi jirani, watu kwa mamia wamekufa kwa imani tete kama hizo. Sasa, bila kutoa risiti, tunakaba

wafanyabiashara huku hawa tukiwaacha, Kwanini? Hivi TRA mnafanya nini?

# PAMBA INAVYOKUWA KIOO CHA NEEMA KWA WAKULIMA KISHAPU KIMAENDELEO

**Na Shaban Njia, KISHAPU**

ZAO la pamba lina umuhimu wa kipekee katika uchumi wa nchi na kwa kiasi kikubwa linategemea zaidi soko la nje, pia linatumiwa na viwanda vya ndani. Uzalishaji uliopo kwa sasa kwa mwaka huu unakadiriwa marobota 300,000.

Takriban ekari 1,500,000 hulimwa na kupandwa pamba kila msimu na katika msimu wa mwaka 2019/2020 zao hilo liliingizia taifa takribani dola za kimarekani milioni 243.07 na hii ni kwa mujibu wa taarifa ya Bodi ya Pamba nchini kulinganisha na mazao mengine ya kibiashara hasa ya zao la Tumbaku.

Pato linalotokana na pamba linaweza kuongezeka mara dufu iwapo kutakuwa na utashi wa kisiasa wa kutaka kuwakwamua wakulima na kusimamia utekelezaji wa kanuni 10 bora za kilimo ambazo wamekuwa wakikumbushwa mara kadhaa na maofisa ugani kila kata lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji.

Shinyanga ni moja kati ya mikoa 17 inayolima zao hilo hasa katika wilaya ya Kishapu kulinganisha na Wilaya nyingine za Shinyanga Vijijini na Kahama, huku Halmashauri yake ikilifanya chanzo cha pili kikubwa cha mapato ya ndani, mbali na mgodi wa almasi wa Mwadui.

Wakulima wake wanaeleza wanavyonufaika nacho, fedha wanazozipata wanazielekeza katika shughuli za maendeleo ndani ya familia zao, ikiwamo kuvuta umeme kupitia Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini(REA) na kuondokana na kutumia vibatari.



Wanawake wakulima wa pamba katika kijiji cha Mtinga, katika Halmashauri ya Bukombe, mkoani Geita, wakifurahia zawadi ya khanga waliyopewa. **PICHA: SHABAN NJIA**

### WAKULIMA PAMBA;

Selina Francis, ni mkulima wa kijijini Butuyu kata ya Bunambiyu, anaeleza ilivyomnufaisha akivuta nishati ya umeme na kuondokana na matumizi ya kibatari.

Anasema, pia analima mazao mengine mchanganyiko, ikiwamo mpunga, alizeti, mahindi na viazi vitamu na fedha anayoipata kwenye pamba, inahudumia familia mahitaji ya shule ya wanafunzi na msimu huu amelima ekari 25.

Agness Mathias anasema, kwenye kata yao wanaolima zao hilo kwa wingi ni wakulima wanawake kulinganisha na wanaume, na kila anapopata fedha anahudumia mabinti zake masomo ya juu cherehani ili kuunda maisha yao.

"Kijiji chetu kilikuwa giza sana na wengi tulikuwa tunatumia vibatari nyakati za usiku, wanafunzi walikuwa wanapata shida sana kujisomea na wengi walikuwa wakilalamika kuumia vifua kwa kuvuta hewa ya moshi wa kibatari, sasa kila kaya imevuta umeme kwa gharama nafuu hakuna malalamiko ya wanafunzi wa kibari" anasema.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi (AMCOS) Butuyu, Shingu Nkanda, anasema ushindani wa bei uliopo baina ya wanunuzi, inawafanya kupata fedha za kutosha, msimu huu mvua zilikuwa nyingi lakini pamba imepatikana japo sio nyingi ila kwa wastani.

Anasema, bei ya serikali kwa kilo moja ni Sh.1,150 lakini wanauza kwa Sh.1,320 sawa na ongezeko la Sh.170, na maeneo mengine wanauza mpaka Sh.1,370 na sasa wanajipanga msimu ujao kulima zaidi kwa sababu wanauhakika wa masomo na bei nzuri tofauti na miaka iliyopita.

### OFISA KILIMO

John Emmanuel, ni Ofisa Kilimo wa Kata ya Bunambiyu, anasema amekuwa akitoa elimu ya namna hiyo katika mikutano ya hadhara anayoitisha kila mwezi na ile ya kisiasa, na wakati mwingine analazimika kumfuata mkulima mmoja mmoja shambani.

Anasema, kata hiyo ina zaidi ya wakulima 3,585 kati yake 1,962 ni wakulima wa pamba na 1,623 ni wakulima wa mazao mchanganyiko ikiwamo mahindi, viazi vitamu, choroko, dengu, alizeti na mpunga, na bei iliyotolewa na kampuni ya ununuzi imewanufaisha wakulima kulinganisha na kipindi cha nyuma.

Anataja a changamoto ya wakulima ni kutokuwa na magunia maalumu yanayohitajika kutumika kuhifadhi pamba kabla na baada ya kuvuna, kwani wengi wanatumia kanga au vitenge kubeba na kuhifadhia, zao linachafuka na kuonekana chafu huku wengine wakitumia mikokoteni ambayo inabeba michanga.

Ofisa kilimo wa kampuni ya ununuzi wa pamba, Jackline Anakleth aliyepo katika kata hiyo anasema, wanashirikiana na serikali katika kuwafikia wakulima na kuwaelimisha kulima kisasa, uvunaji, aina ya vifungashio vinavyotakiwa na uhifadhi ili kuendelea kuwa na pamba bora toka shambani hadi sokoni.

Anasema ni hali inasaidia kuongeza uzalishaji wake na kuwa na pamba ya kutosha nchini kwani katika msimu huu wanatarajia kupitia kata hiyo kupata wastani wa tani 400 za pamba na wanaoongoza kulima zao hilo ni wakulima wanawake kulinganisha na akinababa.

### HALMASHAURI KISHAPU

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kishapu Emmanuel Johnson anasema, Mchango wa Pamba katika mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo ni mkubwa ukilinganisha na mazao mengine yanayozalishwa, mwaka wa fedha 2020/2021 mapato ya ndani yalikuwa Sh. bilioni 1.259 pamba ilichangia Sh. milioni 636.321 sawa na asilimia 50.53 ya mapato yake.

Anasema mwaka uliofuata 2021/2022, mapato ya ndani yalikuwa Sh. bilioni 2.150 pamba ilichangia kiasi cha Sh. milioni 938.558 sawa na asilimia 43.65 huku mwaka 2022/2023 pato la ndani ilikuwa Sh. bilioni 3.157 huku zao la pamba likichangia Sh.milioni 966.347 sawa na asilimia 30.6

Aidha Johnson anasema, mwitikio wa wakulima kulima zao hilo ni mkubwa ikipanda kila msimu kutokana na idadi ya ekari na kilo za uzalishaji zinazoongezeka kila mwaka, na mwaka 2020/2021 ekari 142,024 zililiwa na kilo 14,884,711 zilipatikana na kuuzwa zote sokoni.

Anasema msimu uliofuata wa 2021/2022 ekari 181,657.5 zililimwa na kupatikana kilo 17,605,545 na mwaka uliofuata wa 2022/2023 ekari 200,821.12 zilipatikana kilo za pamba 30,123,168, akinena ni kutokana na elimu ya kilimo cha kisasa wanayopewa na maofisa kilimo waliopo kila kata.

Johnson anasema,wana mikakati wa kuongoza kitaifa kwa kuongeza tija ya uzalisjai kutoka kilo 150 hadi 500 ifikapo 2025/2026, na kila kijiji kinakuwa na Ofisa kilimo ili kuongeza huduma za ugani, mbolea, mbegu na viwatilifu vinapatikana na kuendelea kushirikiana na Bodi ya Pamba na wadau wengine kuhusu usimamizi miongozo, kanuni na sheria zinazosimamia zao hilo.



Wakulima wa pamba katika kijiji na kata ya Buzilayombo wilayani Chato, wakipima pamba wanayotarajia kupeleka sokoni. **PICHA: SHABAN NJIA**



# Wauguzi wamchefua DC kwa lugha chafu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

MKUU wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Thomas Apson amekemea lugha chafu zinazotolewa na baadhi ya wauguzi hospitalini, vituo vya afya na zahanati za serikali wilayani hapa na kusababisha wagonjwa kufa kwa kukosa huduma.

Apson alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha kujadili mpango wa 'tujiongeze tuwavushe salama', mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga (M-Mama), lishe na Bima ya Afya ya Jamii (CHF).

Alisema lugha hizo zinazotolewa na wauguzi hao kwa wagonjwa, pia zinashusha sifa ya wilaya hiyo kutokana na vifo vya wagonjwa kwa kukosa huduma bora za matibabu.

Alisema changamoto ya kauli mbaya dhidi ya wagonjwa imekuwa ikisemwa mara kadhaa hususani katika Tarafa ya Sepuka na kumwomba Ofisa Ustawi wa Jamii wa wilaya hiyo kufuatilia na kuwachukulia hatua wauguzi wanaokiuka taratibu za kazi.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Dorisila John, alisema kila kituo kinapaswa kuhamasisha wananchi na wanafunzi wa shule zote kujiunga na CHF. Dk. John aliagiza waganga wafawidhi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya wa wilaya hiyo kusaidia kutoa elimu ya afya ya uzazi kwenye mikutano ya hadhara na kwa wasichana shuleni na majumbani.

Mfumo wa M-MAMA umezinduliwa katika Mkoa wa Singida mwaka 2022 na kuendeshwa na Serikali kwa kushirikiana na Vodacom.

Kwa mara ya kwanza ulifanyiwa majaribio katika wilaya za Mkoa wa Mwanza na Shinyanga na kufanya kazi kwa ufasaha.



Polisi Kata ya Songe, wilayani Kilindi, mkoani Tanga, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Msaji Mwaswengu akihamasisha ulinzi shirikishi katika mkutano wa hadhara wa wakazi wa kijiji cha Mvungwe, mapema wiki hii. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Wahimizwa kutunza mkongo wa mawasiliano

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ITIGI

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Mnzava, amewahimiza wakazi wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni Mkoa wa Singida kukilinda na kukitunza kituo cha mkongo wa taifa wa mawasiliano kukuza uchumi wao na taifa kwa jumla.

Mnzava alitoa kauli hiyo juzi baada ya Mwenge huo kuzindua kituo hicho kilichojengwa na Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) Kata ya Majengo katika halmashauri hiyo.

"Kituo hiki kitakuwa na msaada mkubwa katika mikoa ya Singida, Tabora, Mbeya na Songwe katika suala la mawasiliano kwa hiyo niwapongeze TTCL kwa ujenzi wa kituo hiki," alisema.

Awali Meneja wa TTCL Mkoa wa Singida, Augustino Mwakyembe, alisema kituo hicho kitaongeza ubora na uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano na mtandao katika taasisi za fedha, serikali, mashirika ya dini na kila mwananchi.

Mwakyembe, alisema pia kitaongeza wigo kwa wawekezaji kwa kupata mtandao na kutoa nafasi kwa watoa huduma wengine.

"Mawasiliano bora yanakuza biashara na huduma mbalimbali, mawasiliano bora yamekuwa kivutio cha wawekezaji katika halmashauri yetu, mawasiliano bora yamechochea usimikaji wa mifumo ya kielektroniki na kutuwezesha kukusanya na kudhibiti makusanyo ya mapato," alisema na kuongeza kuwa:

"Sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwa heshima kubwa tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha Sh. Bilioni 1.3. kwa upande wa kituo cha Itigi pekee kwa ajili ya ujenzi wa mkongo wa mawasiliano."

Aliahidi kukitunza kituo hicho ili kiendelee kuinufaisha jamii na kwa maendeleo endelevu nchini.

Awali msimamizi wa kituo hicho, Hussein Pungu akisoma taarifa ya mradi, alisema kinatoa mawasiliano njia ya Itigi kuelekea Malongwe hadi Tabora na Kiombo, Rungwa hadi mkoani Mbeya.

Alisema mradi huo kwa mujibu wa mkataba ulianza kutekelezwa Februari 4, 2022 na kukamilika Machi 1, mwaka huu ukiwa na kilomita 192 kati ya hizo, 110 (Itigi-Malongwe) na 82 (Itigi-Kiombo) kwa upande wa Itigi. Kwa ujenzi wa nchi nzima una kilomita 4,442 na vituo wezeshi 111, kikiwepo cha Itigi.

# 'Kizazi chenye usawa kijumuishwe dira ya taifa'

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAMATI ya Kitaifa ya Ushauri kuhusu utekelezaji wa Programu ya Kizazi chenye Usawa imeshauri ajenda ya Kizazi chenye Usawa kujumuishwa katika Dira ya Taifa ya 2050 ili utekelezaji wake uwe katika mifumo ya utendaji wa serikali.

Hayo yalibainika wakati wa ziara ya Kamati hiyo kwa Mkoa wa Dodoma juzi yenye lengo la kufuatilia utekelezaji programu hiyo na jitihada zilizopo katika taasisi mbalimbali kukuza haki na usawa wa kiuchumi kwa wanawake nchini.

Akizungumza katika ziara hiyo, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Being'i Issa alisema suala la usawa wa kijinsia ni mtambuka na linahitaji nguvu ya kila taasisi kushirikiana na kuhakikisha linawekwa katika vipaumbele vyake ili kuwezesha kufikia ahadi zilizowekwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kufikia kizazi chenye usawa kiuchumi nchini.

"Niseme tu suala la usawa wa kijinsia sio la Wizara moja au taasisi moja ni letu sote na tukilibeba na kuliweka katika ajenda za Kitaifa litaondoa ukakasi wa ajenda hii kuonekana ni ya upande wa jinsi moja tu bali ni kwa jinsi zote Wanawake kwa wanaume" alisisitiza Being'i.

Mmoja wa wajumbe wa Kamati hiyo Carolyn Kandusi alishauri kuwepo na mikakati dhabiti katika taasisi mbalimbali ili kuwe na mifumo itakayowezesha kuwepo na usawa wa kijinsia katika maeneo muhimu hasa katika sekta zenye kuwezesha wananchi kiuchumi.

# Atangaza mikakati kuongeza mapato madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Madini, Yahya Samamba ameelezea mikakati yake ya kuimarisha sekta ya madini nchini ili kufikia lengo la kuchangia asilimia 10 pato la taifa ifikapo mwaka 2025.

Samamba alitangaza mikakati hiyo juzi baada ya kukabidhiwa ofisi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali baada ya kuteuliwa hivi karibuni kushika wadhifa huo.

Alisema watumishi wa wizara hiyo wanapaswa kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuhakikisha malengo ya Taifa kupitia Sekta ya Madini nchini yanafikiwa.

"Watumishi wenzangu fanyeni kazi kama timu moja muwe na upendo, ushirikiano na amani kuhakikisha malengo ya wizara ya kukusanya Sh. trilioni moja katika mwaka wa fedha 2024/25, utekelezaji wa vipaumbele vyake, utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 na utekelezaji wa Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri yanafikiwa," alisema. Alimpongeza Mahimbali kwa uongozi wake kuleta mafanikio kwenye sekta hiyo, ikiwamo ukusanyaji wa maduhuli ya serikali. "Tunayo majukumu mbele yetu kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la taifa kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025 au kufika mapema kabla ya mwaka huo. Katibu Mkuu Mahimbali ametuacha na asilimia 9.1 ni mafanikio makubwa sana, tuna asilimia 0.9 iliyobaki tuendelee kujiamini tukamilishe. Lakini ili kufikia hapa kila mmoja kwenye eneo lake awasimamie watu wake vizuri," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mahimbali alimweleza Samamba kuwa ana timu nzuri ya kumsaidia kutekeleza majukumu kikamilifu kutokana na ubobezi walionao katika sekta hiyo na kuahidi yuko tayari kusaidia wizara itakapohitaji ushauri wake.





# CCM yaanika mikakati ya ushindi uchaguzi mkuu, mitaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetangaza mikakati mipya ya kupata ushindi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, huku kikisisitiza kuwa kitaendelea kukaa madarakani.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, John Mongela alitaja mikakati hiyo jana jijini Mbeya kwenye vikao na mikutano mbalimbali aliyoifanya na makada wa chama hicho pamoja na watendaji wa wilaya zote za chama mkoani Mbeya.

Mongela alifanya ziara hiyo ya siku moja mkoani hapa kwa lengo la kujitambulisha ikiwa ni siku chache baada ya kuteuliwa na Kamati Kuu ya chama hicho kuwa mlezi wa Mkoa wa Mbeya

Alisema moja kati ya mikakati hiyo ya kuendelea kushinda ni kuwateua wagombea ambao wanakubalika kwa wananchi hasa wale ambao wanashinda kwenye kura za maoni.

Alisema serikali imetekeleza miradi mingi chini ya usimamizi wa chama hicho na hivyo kitahakikisha kinaitumia miradi hiyo kuwashawishi wananchi kuwachagua wagombea wa chama hicho.

Hivyo, alisisitiza kuwa wapo baadhi ya madiwani, wabunge na wenyeviti wa serikali za mitaa na vitongoji ambao hawatekelezi majukumu yao ipasavyo na hivyo kusababisha chama hicho kisikubalike kwa wananchi wa maeneo husika.

"Sisi suala la kushinda kwenye uchaguzi hatuhitaji kujadiliana na mtu, tutahakikisha tunashinda Uchaguzi wa Serikali za Mita ana Uchaguzi Mkuu mwakani, lakini kwa wale viongozi ambao hawatekelezi majukumu yao nawahakikishia kwamba hatutakwenda naye," alisema Mongela. Aliwataka viongozi ambao wapo madarakani wasiwaogope watu ambao wameanza kuzunguka kwa wananchi wakionyesha nia ya kuwania nafasi zao akieleza kuwa wanachotakiwa kufanya ni kutekeleza majukumu yao vizuri ili waaminike.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge alisema chama hicho ni miongoni mwa vyama vinavyofuata misingi ya demokrasia hasa katika upatikanaji wa viongozi wake na kwamba misingi hiyo ndiyo inayosababisha kidumu kwa muda mrefu madarakani.

Alisema wakati wa uchaguzi wa ndani ya chama huwa ni lazima kutokee kutoelewana baina ya pande mbalimbali za wagombea na kwamba akishapatikana mgombea anayewakilisha chama hicho makundi huwa yanavunjwa na unatafutwa ushindi wa CCM. Mwalunenge aliwataka viongozi na wanachama wa chama hicho kuacha kuzalisha migogoro na badala yake wahakikishe wanawaunganisha wanachama wote.

"Uongozi ni kama mbio za kijiti, tutakimbia kwa kupokezana na kama isingekuwa hivyo basi viongozi wetu ambao waliasisi chama hiki mpaka sasa wangekuwa bado wapo madarakani, kwahiyo lazima kiongozi uliyepo madarakani ujuwe kwamba kuna watu watakupokea," alisema Mwalunenge.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela alisema chanzo cha chama hicho kulipoteza Jimbo la Mbeya Mjini kwenye uchaguzi wa mwaka 2010 ilikuwa ni kukosekana kwa mshikamano.

Alisema kukosekana kwa mshikamano huo kulisababisha baadhi ya wanachama wa chama hicho kumpigia kura mgombea wa upinzani ambaye alikuwa ni wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi.

Alisema chama hicho kitahakikisha matatizo hayo hayatokei tena katika jimbo hilo na kwenye majimbo yote ya Mkoa wa Mbeya ili kipate ushindi wa kishindo.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, John Mongela (mwenye skafu), akisalimiana na baadhi ya viongozi wa chama hicho Mkoa wa Mbeya juzi, baada ya kuwasili katika ofisi za CCM, kwa ajili ya ziara ya siku moja. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Shule ya watoto wenye uhitaji kujengwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya inatarajia kujenga shule maalumu ya msingi na sekondari kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Lengo ni kuwapatia fursa ya kupata elimu na kukomesha vitendo vya baadhi ya wazazi na walezi kuwaficha watoto wenye ulemavu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo juzi alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa huo.

Homera alisema mbali na mpango huo wa kujenga shule pia imeandaa utaratibu maalumu wa kuwasaidia mafuta ya ngozi wanafunzi wote wenye ualbino ili kuwanusuru na matatizo ya Ngozi ikiwemo saratani.

Shule hiyo itajengwa katika eneo la Lwambi jijini Mbeya ambako eneo limetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo, huku akidai kuwa shule hiyo itakuwa na miundombinu yote muhimu kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye aina mbalimbali za ulemavu.

"Halmashauri zote za mkoa wetu zimeshiriki kuchangia ujenzi wa shule yetu hii, kila halmashauri imechangia Sh. milioni 50 isipokuwa Halmashauri ya Busokelo ambayo imechangia Sh. milioni 20," alisema Homera.

Alisema kuhusu ugawaji wa mafuta ya ngozi kwa wenye ualbino alisema watashirikiana na Chama cha Watu wenye Ualbino ili kuwabaini wanafunzi hao shule wanazosoma.

Vilevile, alisema mkoa huo unaendelea na ujenzi wa Shule ya Sayansi ya Wasichana katika Wilaya ya Kyela na kwamba mradi huo upo katika hatua za mwisho kukamilika.

# RC aagiza wafugaji kuchukuliwa hatua

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuwachukulia hatua kali wafugaji watakaoingiza mifugo kwenye Skimu ya Umwagiliaji ya Itipingi, akidai kuwa inaharibu miundombinu ya skimu hiyo.

Aidha, ameagiza kutungwa sheria na adhabu zake haraka na kubandikwa katika maeneo yote ya umma ikiwemo makanisani, misikitini, ofisi za vijiji pamoja maeneo ya wazi ili kila mwananchi azione.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati wa kumkabidhi mkandarasi Sihotech Engineering Co. Ltd & Amt Global Multicontractors Company Ltd eneo la mradi wa umwagilaji Itipingi lenye thamani ya Sh. bilioni 5.2.

Mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha wananchi 417 wa eneo hilo ambao na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa chakula pamoja na kipato kwa wananchi wa eneo hilo.

Mtaka alisema kuwa kila mwananchi mwenye mifugo yake afuge kwenye eneo lake ambalo ni nje na mradi huo pamoja na maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji.

"Serikali imeleta Sh. bilioni tano tusahau kuhusu kuleta ng'ombe hapa kwenye eneo la mradi na wala kusiwe na lugha mbadala, viongozi wa kijiji mtengeneze sheria ya kulinda eneo la mradi wa umwagiliaji dhidi ya vitendo vya mifugo na adhabu zake," alisema Mtaka.

Alisema ni lazima mambo hayo ya sheria yawe katika mfumo ili yapitishwe pamoja na kusimamiwa kwa ajili ya kulinda mradi huo usiharibiwe.

Mhandisi wa umwagiliaji kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), Machage Mwema alisema eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni zaidi ya ekari 820 lenye wanufaika zaidi ya 417.

Aliwataka wananchi hao kutoshiriki kuhujumu mradi huo kwa kutofanya vitendo vya wizi wa vifaa vya ujenzi kwa sababu jambo hilo litasababisha kumkwamisha mkandarasi, hivyo kushindwa kukabidhi mradi kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Sihotech Engineering Co Ltd & Amt Global Multicontractors Company Ltd, Adamu Sikigoye aliwaahidi wananchi hao kwamba wataanza haraka kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kuweza kutekeleza mradi huo kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema mradi huo umekuja wakati sahihi na siyo nadharia bali ni fursa kwa wananchi kwa sababu utapandisha thamani ardhi yao pamoja na maisha.



# Mbunge ataja siri mafanikio ya miradi jimboni kwake

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MBUNGE wa Kojani Mkoa wa Kaskazini Pemba, Hamad Hassan Chande amesema ushirikiano uliopo kati yake na viongozi wa jimbo hilo umewezesha miradi aliyoianzisha kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Alisema kufanikiwa kwa miradi hiyo kumemuwezesha kutekeleza ahadi alizoziweka kwa wananchi wa jimbo hilo kwa zaidi ya asilimia mia katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Aliyasema hayo Kinyikani Mchanga Mdogo Wilaya ya Wete Pemba alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya tathmini ya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo jimboni humo.

Alisema kuwa ziara yake jimboni humo imekuwa ya mafanikio makubwa kwa vile ameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo kwa kiwango kilichohitajika.

Chande alisema ni mradi mmoja tu wa ujenzi wa Shule ya Maandalizi Kiwani Mchangamdogo hakuridhika nao ambapo alitoa maelekezo ya kufanyiwa marekebisho.

Alisema ujenzi wa shule hiyo ambao ukimalizika utaondoa changamoto ya watoto wadogo kufuata masomo umbali wa kilomita tatu.

Alisema Sh. milioni 67 zimeshatumika, akidai mfuko wake wa jimbo una Sh. milioni 83.

Mbunge alisema hamu na shauku yake ni kuona miradi inayotekelezwa ndani ya jimbo lake imakamika kwa viwango vilivyotakiwa.

Hivyo, aliwataka makandarasi wa ujenzi wa miradi ndani ya jimbo lake wahakikishe wanapopewa kazi wajenge kwa viwango bora na viendane na thamani ya fedha wenyewe.

Alisema inasikitisha kuona baadhi ya miradi hailingani na gharama za ujenzi, hivyo aliwataka makandarasi wa ujenzi wa shule hiyo kuhakikisha mwishoni mwa mwezi huu ujenzi huo unakamilika.

# Dk. Mwinyi: Tutaboresha mazingira ya biashara, uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuwa rafiki zaidi.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la uwekezaji wa visiwa vidogo Zanzibar, ambalo limeandaliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), kwa kushirikiana na mradi wa USAID Heshimu Bahari.

Alisema Serikali ya Zanzibar kupitia ZIPA na taasisi nyingine za serikali zinazohusika na uwezeshaji wa uwekezaji zitaendelea kushirikiana na wawekezaji katika kuhakikisha miradi hiyo.

Dk. Mwinyi alisema hatua ya kukodisha visiwa kwa uwekezaji wa muda mrefu ulikuwa uamuzi wa kimkakati ambao ulisababisha usajili wa miradi 16 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 384 na inatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 7,000 kwa wenyeji.

Aidha, alisema ni matarajio yake kuwa kongamano hilo litakuwa na jukumu muhimu katika kuwashauri wawekezaji na wale ambao wana shughuli zao za kila siku kuzunguka visiwani ili kuelewa umuhimu wa kuhifadhi na kulinda rasilimali hizo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi.

Alisema Zanzibar inajulikana kwa mazingira mazuri ya baharini, miamba ya matumbawe yenye nguvu na maisha tofauti ya baharini.

"Mali hizi za asili siyo tu chanzo cha fahari kwa taifa letu bali pia ni sehemu muhimu ya uchumi wetu, hasa kupitia utalii na uvuvi" alisema. Dk. Mwinyi alisema kuna changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira, hivyo ni muhimu ziwepo juhudi za pamoja ili kuhifadhi na kulinda rasilimali hizo muhimu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif alisema uwekezaji wa visiwa unakwenda vizuri na kuleta tija ambayo itapatikana katika uwekezaji huo, ikiwemo ajira, mapato yatokanayo na watalii watakaofika katika visiwa hivyo.

Alisema serikali ina mpango wa kuwaondoa wawekezaji ambao wamekodi visiwa lakini kwa muda mrefu hawajaviendeleza wala kufanya uwekezaji wowote na kuwapa wawekezaji ambao wapo tayari.

Mkurugenzi wa ZIPA, Saleh Saad Mohamed alisema visiwa 17 tayari vimeshawekezwa na kampuni 16 zenye mtaji wa Dola za Marekani milioni 385.4.

Alisema utaratibu wa ukodishwaji wa visiwa hufanya na ZIPA lakini hushirikiana na taasisi mbalimbali za kiserikali ikiwemo Wizara ya Utalii na Idara ya Mazingira.

Alisema pia wawekezaji wote wa visiwa lazima washirikiane na wanajamii wa maeneo hayo ikiwemo wavuvi ili kuendelea kufanya shughuli zao za kujitafutia kipato.

Mratibu Mkuu wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Bahari, Dk. Mathias Igulu alisema uwekezaji unaofanyika katika visiwa unalenga kuhifadhi mazingira kwa faida ya wanajamii, serikali na wawekezaji.

Alisema lazima kuwepo na mifumo ya kusimamia uhifadhi wa mazingira katika visiwa na kuahidi kuwa watasaidia katika suala zima la uhifadhi bahari.



Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (kulia) akifafanua jambo kwa Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa kampuni ya Choplife IP, Oluwagbemiga Odeneye, kuhusu kiatu maalumu kinachotumika katika matibabu ya ulemavu wa mguu kifundo, walipotembelea hospitalini hapo, Msasani Dar es Salaam jana, kujionea kazi na huduma zitolewazo pia kuangalia maeneo wanayoweza kushirikiana ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma bora za afya kwa Watanzania. Kushoto ni Meneja Mkazi wa Choplife Foundation Tanzania, Loyce Oluoch. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali kufanya mageuzi sekta ya kilimo,mifugo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa amesema serikali inampango wa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo na mifugo, ili kuongeza uzalishaji zaidi.

Aliyasema hayo Zanzibar wakati akiwapokea madaktari bingwa wa kilimo na mifugo 23 waliomaliza masomo yao ya miaka minne katika Chuo Kikuu cha Yichun nchini China na kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Alisema kuna uhitaji mkubwa wa vyakula hasa nyama ya kuku, ng'ombe, hivyo wanahitaji wataalamu hao waje na njia bunifu za kisasa kuiondoa Zanzibar hapa ilipo.

"Hii ni changamoto kubwa kwa sababu unakuta tunasafirisha kuku wengi kutoka nje, hivyo wataalamu hawa ni tegemeo letu kuwa wataisaidia serikali kuliondoa tatizo hilo", alisema.

Alisema Zanzibar kuna hoteli zaidi ya 600 lakini nyama zote zinazouzwa kwenye hoteli hizo zinatoka nje ya Zanzibar.

"Lakini Zanzibar hii inasifika sana kwa viungo pamoja na karafuu, wataalamu nyinyi mtusaidie kupambana na wadudu waharibifu ili vitu vyao hivyo viweze kuuzika, viwe na ubora", alisema.

Alisema hatua ya serikali kusomesha wataalamu hao lilikuwa ni agizo la serikali ambapo na wao Wizara ya Elimu ni wasimamizi na kwamba walilitekeleza kwa vitendo.

Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Iddi Khamis alisema wanafunzi hao walikuwa 25 lakini wawili walikwama njiani na kushindwa kuendelea.

Alisema kuwasomesha vijana hao lilikuwa ni agizo la serikali kutokana na kuwepo upungufu mkubwa wa wataalamu hao.

Alisema madaktari waliopokelewa ni awamu ya mwisho kutoka China na waliobakia wawili wapo Urusi na wengine walipelekwa Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Alisema wanafunzi hao wamesomeshwa kwa njia ya mkopo na kila mmoja ametumia Sh. milioni 39, fedha ambazo watazirudisha baada ya kupewa ajira.

Aidha alisema kuwa ujio wao utaongeza idadi ya madakrati wa wanyama ambao watasambazwa katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba, ili kutoa huduma kwenye maeneo hayo.

Mkurugenzi wa Utumishi kutoka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Noah Saleh Said, alisema kuwa asili na chimbuko la kusomesha madaktari hao lilitokana na agizo la Rais Mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein ambaye alisema Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa madaktari, kuagiza limalizwe haraka.

Alisema Zanzibar ilikuwa na madaktari bingwa wa wanyama wawili, baada ya kuhitimu hao watakuwa na madaktari 63.

Wakizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzao, Saleh Abdalla Habib na Aisha Mikidadi Simai waliishukuru serikali kupitia Wizara ya Elimu na Wizara ya Kilimo kwa kuwasomesha ili kukuza ustawi wa elimu.

# Nchimbi aonya viongozi kutoa kauli za kibaguzi

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi amewataka viongozi na wanachama wa CCM kuepuka kutoa kauli au kufanya vitendo vyenye taswira inayoweza kutafsiriwa kuwa baadhi yao wanashabikia ukandamizaji wa haki za wananchi.

Amesisitiza kuwa maneno na vitendo vya wana-CCM wakati wote lazima yaakisi dhamana ambayo chama kimepewa na wananchi ya kuwatumikia, ikiwamo kusimamia haki, bila ubaguzi wala dhuluma ya aina yoyote.

Balozi Nchimbi alisema hayo jana akiwa Chuo cha Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Ihemi, mkoani Iringa, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji na viongozi wa jumuiya hiyo wa ngazi za mikoa na wilaya zote nchini.

"Suala jingine ninataka kuwasisitiza UVCCM ni umuhimu wa watendaji wetu, viongozi wetu na wanachama wetu kutambua kuwa mnabeba taswira ya chama chetu kila wakati, katika mnayosema au kutenda.

"Kama kuna jambo tunapaswa kulilinda kwa wivu mkubwa ni taswira chanya ya CCM, hasa jambo linalohusu dhamana ya kuongoza nchi yetu na kuwatumikia wananchi kwa haki na usawa, kwa kupinga kauli na vitendo vya ubaguzi na dhuluma kwa Watanzania.

"Ninyi UVCCM mnapaswa kuwa mstari wa mbele katika kulinda taswira hiyo muda wote. Tujiepushe kabisa na kauli au matendo yanayoharibu taswira ya CCM. Katika kila unachokisema au kukitenda lazima utafakari, je kina athari gani kwa CCM na nchi yetu," alisema.

Balozi Nchimbi alisema katika kulinda dhima hiyo ya CCM, amewakumbusha wana-CCM na Watanzania kwa ujumla kuwa hadi sasa hakuna chama kingine tofauti na chama tawala.

Alisema CCM kimeonesha uwezo wa kuongoza nchi na wananchi hawako tayari kufanya majaribio kwa vyama vingine ambavyo havina mwelekeo, hali ambayo ni hatari kwa uimara wa nchi

Balozi Nchimbi aliwapongeza UVCCM kwa kuweka 'rekodi' mpya ya kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa walipozindua mkakati wao wa 'Tunazima Zote, Tunawasha Kijani' akiwataka wasonge mbele.

Pia, aliwataka watumie ushawishi walionao kwa vijana nchini, kwa uaminifu na uadilifu, huku wakitambua kuwa Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan, ana imani kubwa na vijana.

Awali akimkaribisha Balozi Nchimbi, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohammed Ali Mohammed (Kawaida), alikishukuru chama hicho chini ya Mwenyekiti Rais Samia kwa namna kinavyoendelea kuwalea na kuwaamini vijana kukitumikia chama na jumuiya zake nchi nzima.

Katibu Mkuu wa UVCCM, Joketi Mwegelo, katika taarifa yake kuhusu maandalizi ya mafunzo hayo, alisema yatawasaidia viongozi na watendaji wa jumuiya hiyo kwenye mikoa, wilaya na hatimaye kushuka ngazi zingine nchi nzima kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi unaohitajika.



# Mombo ateuliwa Mkurugenzi Mkuu Usalama wa Taifa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua na kumwapisha, Suleiman Mombo, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Sharifa Nyanga Ikulu, kabla ya uteuzi huo Mombo alikuwa Ofisa Mwandamizi wa Ofisi ya Rais, Ikulu.

Taarifa hiyo ilisema Mombo amechukua nafasi ya Balozi Ali Siwa ambaye amestaafu.

Agosti 28, mwaka jana, Rais alimteua Siwa kushika nafasi hiyo baada ya mtangulizi wake, Said Massoro, ambaye aliteuliwa kuwa Balozi.



# Rais Samia kuanza ziara Katavi

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajia kuanza ziara ya kikazi mkoani Katavi ikiwa ni mara ya kwanza kutembelea mkoa huo tangu aingie madarakani mwaka 2021.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi kwa umma na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ziara hiyo ya siku nne itaanza leo na atazindua miradi mbalimbali ya maendeleo na kufanya mikutano ya hadhara.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko jana akitoa taarifa ya ujio huo, akisema kuwa Julai 12, mwaka huu, Rais Samia atatembelea jengo la abiria.

Mwamvita alisema pia, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika kilele cha wiki ya Jumuiya ya Wazazi kitaifa itakayofungwa rasmi Julai 13, mwaka huu, katika uwanja wa CCM Azimio Manispaa ya Mpanda.

"Katika kilele cha maazimisho ya wiki ya wazazi, Rais Samia atazungumza na wananchi wa Mkoa wa Katavi kupitia mkutano wa hadhara," alisema Mrindoko.

Vilevile, alisema atakagua kituo cha kupozea umeme wilaya ya Mlele ambacho umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Mkoa wa Tabora utapokewa na kupozwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Alisema Jumapili atafungua jengo jipya la Ofisi ya Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi na kufanya uzinduzi wa maghala ya kutunzia mazao katika eneo la Mpanda Hotel yanayomilikiwa na taasisi ya serikali ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuzindua Bandari ya Karema.

Alisema Jumatatu anatarajiwa kutembelea ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya mkoa huo na kufanya mkutano wa ndani wa majumuisho na viongozi mbalimbali, kisha ataondoka kuelekea mkoani Rukwa.

Alisema njiani atasalimiana na wananchi wa kijiji cha Kibaoni Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, hivyo amewaomba wananchi wa Mkoa wa Katavi kuendelea kuimarisha amani na utulivu na kujitokeza kwa wingi kumpokea.

Katika video fupi iliyoko katika mitandao ya kijamii inaonesha baadhi ya wananchi ambao ni wafanyabiashara wadogo na madereva bodaboda wakieleza kufurishwa na ziara ya kiongozi huyo mkoani humo.

"Tunashukuru sana tuna mkaribisha, hitaji letu aendelee kutuimarisha katika biashara zetu," alisema mmoja wa wafanyabiashara ndogo katika moja ya masoko mkoani humo.

"Rais wetu mpendwa tunakukaribisha sana Katavi. Tunashukuru sana kwa ujio wake Katavi kwa kuwa tangu tupate mkoa hatujapata ugeni mkubwa kama huu. Tutampokea vizuri na tutakuja kwa wingi," alisema mwananchi mwingine.

"Tunamuomba aendelee kutuimarisha pia atuangalie tupate soko kubwa na kuimarisha biashara zetu," alisema mwananchi huyo ambaye hakutaja jina lake.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) Neema Hussein (KATAVI)**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**HAMZA AHMED MAKAME**

anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 307 CLA, MC 187 CAM , MC 493 BYX, MC 769 CEY** . kwa yeyote atakaezıona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/TAN/TAN/4878/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PATRICK ONESPHARD MUNISI**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki(San Lg) yenye namba za usajili T 220CUB, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/22017/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**SELEMAN SAID ABDALLAH**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya Isuzu yenye usajili T686 ARC. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae.

TAARIFA YA POLISI.

**PHQ/TAN/MKI/7006/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABEID SALUM ABEID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0884-0501** kilicholewa na **MAMBWE SEKONDARI** Mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/140083/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUD JAPHET MATHAYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S3804-0624 kilicholewa na **MUHEZA HIGH SCHOOL** Mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MKI/7018/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELLYGLORY NICHOLAS KOMBE** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo cha Uuguzi (NTA level 5) chenye namba NS1037/0007/2010 kilichotolewa na Kairuki School of Nursing mwaka 2018.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/TAN/7036/2024.**

HABARI KIMATAIFA

# Ruto avunja baraza la mawaziri

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, amelivunja baraza lake la mawaziri na kumbakisha Musalia Mudavadi kuendelea na na nafasi yake.

Mudavadi anaendelea na kazi yake ya Kiongozi wa mawaziri na Waziri wa Masuala ya Kigeni.

Katika tangazo lake, Ruto alisema hatua aliyochukua ni muhimu kwa taifa wakati akichukua muda kufanya majadiliano ya kuunda baraza jipya la mawaziri litakalohusika na uendeshaji wa serikali.

"Mara moja nitashiriki katika mashauriano ya kina katika sekta mbalimbali ikiwamo ya kisiasa, kwa lengo la kuunda serikali pana ambayo itanisaidia katika kuongeza kasi na kuharakisha yanayohitajika," alisema Ruto.

Alisema hatua hiyo itakuwa ya haraka pamoja na utekelezaji wa mipango madhubuti ya kukabiliana na mzigo wa madeni unaloikumba taifa hilo.

Pia matatizo yatakayoangaliwa kwa utekelezaji ni kuongeza rasilimali za ndani, kupanua nafasi za kazi,kuondoa uharibifu wa fedha, kuondoa msururu wa vyombo vya serikali vinavyofanana na kupambana na ufisadi.



Rais Ruto alisema wakati akiendelea na mchakato wa kuliteua baraza jipya la mawaziri ,shughuli za serikali zitaendelea bila kuvurugwa chini ya uongozi wa Makatibu wakuu na maofisa wengine.

Kiongozi huyo alisisitiza kwamba uamuzi huo umechukuliwa baada ya matukio ya maandamano ya hivi karibuni ambayo yalilazimu kuondolewa kwa Muswada wa Fedha wa 2024.

"Nimechukua hatua hii baada ya kutafakari, kusikiliza Wakenya na tathmini ya jumla ya baraza langu la mawaziri".

Katika hotuba yake aliyoitoa Ikulu ya Nairobi, Rais Ruto alitangulia kwa kueleza baadhi ya mafanikio ya serikali yake yaliyopatikana kwa muda wa miaka miwili ikiwemo kupunguza mfumuko wa bei, kuifanya uthabiti wa shilingi ya Kenya dhidi ya dola ya Marekani, kuunda nafasi zaidi za ajira kupitia vituo vya kidijitali na mpango wa ujenzi wa nyumba na kupunguza bei ya mbolea kwa wakulima .

Gen Z ilishinikiza serikali kuwajibika zaidi kupitia utawala bora na matumizi mazuri ya fedha za umma na kuukataa muswada wa fedha.

Siku chache zilizopita, Rais Ruto alitangaza hatua mbalimbali za kupunguza matumizi ya serikali ikiwemo kuondoa bajeti kwa ofisi za mke wa rais, mke wa naibu wa rais na mke wa kiongozi wa mawaziri.

Awali, akiwa kaunti ya Kajiado, kiongozi huyo aliyashutumu mataifa ya kigeni akidai kufadhili maandamano nchini mwake.

"Wale wanaojaribu kufanya mambo katika kupanga (maandamano), sijui wapi kupanga mambo ya nini, mimi nataka niwaambie Kenya ni taifa la kidemokrasia na hii ni nchi yetu na hatuhami," alisema.

Akijibu shinikizo la kumtaka kuondoka madarakani kutoka kwa vijana wa Gen z, Rais Ruto alisema Wakenya watapata fursa ya kutoa uamuzi wao katika Uchaguzi Mkuu ujao wa 2027.

Alisisitiza kuwa hakuna njia za mkato na kwamba raia wanapaswa kusubiri uchaguzi ujao ili kuwachagua viongozi wapya.

"Kwa hiyo, hakuna haja ya kurejesha nyuma amani ya nchi, hakuna haja ya kutumia njia ya mkato, hakuna haja ya kutumia njia ya mkato. Wananchi hawa ni werevu na ndio wataamua jinsi Kenya itasonga mbele," alisema. **BBC**

## Rwanda iko tayari kuwapokea wahamiaji kutoka nchi zingine

**KIGALI,** Rwanda

Rwanda inalenga kuzishawishi nchi za ulaya zilizoelemewa na wahamiaji kuwahamishia katika ardhi yake, baada ya mpango kama huo uliotiwa saini na serikali ya Uingereza kufutwa.

Serikali mpya ya Uingereza inayoundwa na Chama cha Labour, ilifuta mpango wa kuwapeleka wahamiaji Rwanda, kama kutimiza ahadi yake wakati wa kampeni.

Uingereza ilifuta makubaliano hayo yenye utata na Rwanda, kutokana na malalamiko kutoka kwa watu wengi akiwamo Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia wakimbizi.

Serikali ya Rwanda tayari ilikubali kuwapa hifadhi karibu wakimbizi 100,000, na kulipwa kiasi cha euro milioni 300 ambazo hazitarudishwa.

Kulingana na Naibu Msemaji wa Serikali ya Rwanda, Alain Mukuralinda, licha ya kutotekelezwa makubaliano hayo, nchi yake inaendelea kujitolea katika suala la mzozo wa uhamiaji.

"Siku zote tuko tayari kuchunguza masuluhisho mengine ambayo yanaweza kuokoa maisha ya binadamu, na mradi bado kuna waathiriwa na hakuna masuluhisho mengine, serikali ya Rwanda daima itakuwa wazi kwa njia nyingine ya kutatua tatizo hilo," alisema.

Alisema nchi zingine kama Denmark zilionyesha nia ya kuingia makubaliano kama hayo.Hata hivyo mazungumzo hayo yamesitishwa.

"Hakuna majadiliano zaidi. Lakini kama unavyojua, kabla ya Uingereza, kulikuwa na nchi nyingine za kaskazini, lakini hakuna majadiliano zaidi ," aliongeza kusema msemaji huyo.

Aliongeza kwamba ikiwa nchi nyingine zitafanya hivyo, Rwanda haitakataa ombi lao kutokana na falsafa yo haitabadilika.

Alisisitiza licha ya mpango huo kukwama, Rwanda haina jukumu la kurudisha pesa hizo ambazo tayari Uingereza imelipa kutumika kwa ujenzi na miundombinu ya mapokezi. **RFI**




Vifaru vya Israel vikiuzingira mji wa Gaza kujiandaa na mashambulizi mapya. **PICHA: UPI**

# Umoja wa Mataifa wapinga Wapalestina kuhama Gaza

**NEW YORK,** Marekani

UMOJA wa Mataifa umepinga amri ya jeshi la Israel ya kuwataka raia wanaoishi mji wa Gaza kuondoka haraka ili kuepusha madhara.

Katika taarifa iliyotolewa jana, Umoja wa Mataifa ulisema hatua hiyo itasababisha mateso kwa wakazi hao ambao kwa sasa wanahangaishwa kutokana na mashambulizi yanayoendelea.

Amri hiyo inatafsiriwa na waangalizi wa mzozo huo kuwa ni ishara ya kuanza operesheni mpya za kijeshi za Israel katika Ukanda huo.

Ofisi ya kuratibu masuala ya kiutu ya Umoja wa Mataifa OCHA, ilitoa onyo hilo katika taarifa iliyoitoa Jumatano ikisema kuwa maelekezo yaliyotolewa na Israel ya kuwataka watu waondoke mjini Gaza yatachochea madhila makubwa kwa familia za Kipalestina ambazo zimekuwa zikilazimika kuhama hama mara nyingi kutokana na vita.

Jeshi la Israel limedondosha maelfu ya vipeperushi kwenye mji wa Gaza ambao kulingana na Umoja wa Mataifa unakaliwa na wakazi 350,000.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Stephen Dujarric, amebainisha kwamba raia wanapaswa kulindwa na kupatiwa mahitaji yao bila kujali kuwa wanakimbia maeneo yao au la.

Dujarric pia alifafanua kuhusu njia ambazo wanatakiwa watu hao kupita bila kukaguliwa kuwa ni hatari.

Msemaji huyo alitoa wito kwa pande zote zinazohusika kwenye mzozo kuheshimu sheria ya kimataifa kuhusu masuala ya kiutu.

Wakati huo huo jeshi la Israel lilisema juzi kuwa limekamilisha shughuli kwenye eneo la Shujaiya, mashariki mwa Gaza.

Eneo hilo ambalo limekuwa uwanja wa mapambano kwa muda wa wiki mbili, Israel ilidai ilifanikiwa kuyaharibu mahandaki mawili na kuwaua magaidi kadhaa.

Israel ilianzisha mashambulizi mwanzoni mwa mwezi Mei katika eneo la wa Rafah linalopakana na Misri likilitaja kuwa ni ngome ya kundi la Hamas.

Kuanzia mwezi huo, mapigano yameongezeka kati ya wanajeshi hao na wanamgambo wa Hamas kaskazini na katikati mwa Ukanda wa Gaza. **DW**

# KIPRE JR ASAINI MIAKA MINNE MC ALGER

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Azam FC jana umethibitisha kumuuza nyota wake raia wa Ivory Coast, Kipre Jr kwenye klabu ya MC Alger ya Algeria ambako amesaini mkataba wa miaka minne kuwatumikia waarabu hao.

Awali kulikuwa na tetesi za muda mrefu zikimuhusisha nyota huyokutaka kuondoka klabunihapobaadayakupata dili kubwa nje ya Tanzania.


**Hata hivyo mara kwa mara klabu ya Azam ilikuwa ikikanusha taarifa hizo za tetesi mpaka juzi jioni walipothibitisha kumuuza mchezaji huyo.**

Taarifa ya klabu hiyo imesema wamefikia makubaliano na klabu hiyo na kufikia maamuzi ya kumuuza kiungo huyo mshambuliaji.

"Tumefikia makubaliano na klabu ya MC Alger ya Algeria kumuuza kiungo mshambuliaji wetu, Kipre Junior.

"Kipre Jr, tayari ameshasaini mkataba wa miaka minne na klabu hiyo baada ya kufaulu vipimo vya afya," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, Azam FC imemshukuru mchezaji huyo kwa mchango wake ndani ya klabu hiyo kwa misimu yake miwili na imemtakia kila la kheri katika klabu yake mpya.




Mchezaji wa zamani wa Azam FC, Kipre Jr akiwa kwenye jezi ya timu yake mpya ya MC Alger ya Algeria muda mfupi baada ya kutambulishwa jana. **PICHA:BINZUBEIRY**

## Waogeleaji olimpiki kwenda Ufaransa

**Na Shufaa Lyimo**

WAOGELEAJI wawili wa Tanzania, Sophia Latiff na Collins Saliboko wanatarajia kuondoka nchini Julai 23 kwenda Paris, Ufaransa tayari kushiriki michezo ya Olimpiki itakayoanza Julai 26 nchini humo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Habari wa Chama cha mchezo wa kuogelea Tanzania (TSA), Sebastian Kolowa, alithibitisha safari hiyo na kusema waogeleaji hao wanaendelea na mazoezi kila siku kwenye bwawa la kuogelea lililopo kwenye Shule ya Kimataifa Tanganyika( IST), Masaki, jijini Dar es Salaam.

„Maandalizi yanaendelea vizuri kwa wachezaji wetu, wanafanya mazoezi wakiwa chini ya Kocha Mkuu, Alexander Mwaipasi, tunaimani watakwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa," alisema Kolowa.

Kwa upande wake Sophia alisema malengo yake ni kwenda kutengeneza rekodi mpya katika mashindano hayo kwa kuhakikisha anapata medali nyingi.

„Nataka kuweka rekodi mpya, nitahakikisha ninafuata maelekezo ninayoendelea kupewa na Kocha wangu wakati nikiwa kwenye mazoezi," alisema Sophia.

Alisema kwa upande wake yeye ataanza kuogelea Agosti 3 mwaka huu hivyo kuomba watanzania wamuombee ili akatimize malengo yake.

Aidha aliwataka wasichana kujitokeza kwa wingi kujifunza mchezo huo kwani ni mchezo wa kawaida kama ilivyo michezo mingine.

Alisema amekuwa akipata mafanikio kwenye mchezo huo kutokana na ushirikiano anaoupata kutoka kwa familia yake, uongozi wa TSA pamoja na marafiki.

# Mwenda aanza kwa kasi Coastal Union

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonyesha kuwa usajili mpya wa Coastal Union umeanza kulipa mchezaji mpya wa timu hiyo, Ramadhani Mwenda ameanza kwa kasi kwenye kikosi cha timu hiyo baada ya kufunga bao moja muhimu kwenye michuano ya Dar Port Kagame Cup inayoendela jijini Dar es Salaam.

Mwenda, aliyejiunga na Coastal Union akitokea klabu ya KCB ya Kenya, alifunga bao hilo la pekee kwenye mchezo dhidi ya Dekadaha ya Somalia kwenye uwanja wa Manispaa ya Kinondoni.

Coastal Union inayatumia mashindano hayo ya Klabu bingwa Afrika Mashariki na Kati kama sehemu ya maandalizi kwa ajili ya Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki msimu ujao.

Hata hivyo, katika mchezo wao wa kwanza dhidi ya Wasomali hao, beki wao tegemeo, Lameck Lawi, alikuwa jukwaani akiwatazama wenzake wakicheza na kuzua maswali mengi kutoka kwa mashabiki.

Mchezaji huyo ambaye alitangaza kusajiliwa na Simba, lakini Coastal ikapinga usajili huyo, habari zinasema suala lake kwa sasa lipo kwenye vyombo vya sheria hivyo inadaiwa hawezi kucheza hadi suala lake litakapomalizika.

Uongozi wa klabu ya Simba umesisitiza mchezaji huyo nimali yao baada ya kukamilisha usajili, huku upande wa Coastal Union ukisema Simba walikikuka makubaliano na hivyo mchezaji huyo bado ni mali yao.

Inaelezwa ‚Wagosi wa Kaya' wamerejesha fedha walizoingiziwa kwenye akaunti yao ya benki na Simba kama malipo ya kumsajili beki huyo wa kati.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEVES AGOMBEWA ULAYA
KLABU ya PSG iko tayari kushindana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka, 19 Joao Neves. (***Le10Sport***)

### WILLIAMS MAMBO SAFI BARCA
BARCELONA imefikia makubaliano ya kimsingi kwa mshambuliaji wa Athletic Bilbao na Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 21. (***Sport***)

### DE LIGT AKARIBIA KUTUA UNITED
KLABU ya Manchester United ina nia ya kukamilisha usajili wa beki wa Bayern Munich, Mholanzi Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24, haraka iwezekanavyo baada ya Euro 2024. (***Bild***)

### NUNO TAVARES HUYOO ARSENAL
ARSENAL imekubali ofa ya mkopo kutoka kwa Lazio kwa beki wao wa pembeni wa Ureno, Nuno Tavares mwenye miaka 24 na kulazimika kumuuza kati ya pauni milioni 6. (***Mirror***}

### CHELSEA HAINA MPANGO NA OLMO
CHELSEA haina nia ya kuanzisha mazungumzo ya kumnunua mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 26 kutoka katika klabu yake ya RB Leipzig kwa pauni milioni 50. (***Sky Sports***)

### GREAVES MAMBO SAFI IPSWICH
MLINZI wa kati wa England, Jacob Greaves mwenye umri wa miaka 23, amekamilisha matibabu yake ya kuhamia Ipswich Town kutoka Hull City. ***(Sky Sports)***,

### RABIOT HURU KUONDOKA JUVENTUS
LIVERPOOL, Bayern Munich au Real Madrid huenda ndiko anakoelekea kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29 ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Juventus kumalizika mwezi uliopita. ***(Calciomercato)***

### EDDIE NKETIAH ATAKIWA MARSEILLE
MARSEILLE ianavutiwa na mshambuliaji wa Arsenal na England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25. (***Footmercato***)

### SIMONS AWANIWA BAYERN MUNICH
KLABU ya Bayern Munich inataka kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21, kutoka Paris St-Germain. (***Sky Sports***)

### MONACO YAIWEKEA NGUMU FOREST
MONACO imekataa dau la euro milioni 30 kutoka kwa Nottingham Forest kwa ajili ya kiungo wa kati wa Ufaransa, Youssouf Fofana mwenye umri wa miaka 25 ambaye amekubali makubaliano na AC Milan. (***Fabrizio Romano)***




# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# PALHINHA ATUA RASMI B. MUNICH

**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO wa Ureno, Joao Palhinha amekamilisha uhamisho wake kwenye klabu ya Bayern Munich.

Taarifa ya mwandishi wa habari za michezo maarufu, Fabrizio Romano imeeleza kuwa Palhinha amesaini mkataba wa miaka minne utakaomuweka klabuni hapo hadi 2028.

**Wiki iliyopita Palhinha alikamilisha vipimo vya afya ili kujiunga na Bavaria hao.**

Fulham itapokea euro milioni 50 kwa uhamisho huo.

Romano amesema Bayern itamtangaza Palhinha baada ya kumtangaza Michael Olise kisha timu hiyo itaendelea na uhamisho wa Jonathan Tah.

Palhinha alijiunga na Fulham akitokea Sporting CP ya Ureno baada ya kuitumikia Braga na Belenenses za nchini humo kwa mkopo.

Usajili wa kiungo huyo utakuwa wa pili baada ya Olise wiki iliyopita kutua jiji la Munich kukamilisha usajili wake.

●●● Wababe hao wa Ujerumani wanatarajia kumtangaza nyota huyo baada ya....

# SOUTHGATE: KUFIKA FAINALI YA MAFANIKIO YANGU BORA



**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA Gareth Southgate amesema kuwa kuiongoza England kwenye fainali ya kwanza ya michuano mikubwa katika ardhi ya kigeni ni mafanikio bora zaidi katika maisha yake ya ukocha.

Mchezaji wa akiba Ollie Watkins alifunga bao la ushindi dakika ya 90 wakati England ikitoka nyuma na kuilaza Uholanzi 2-1 huko Dortmund na kutinga fainali ya euro watakayocheza na Hispania mjini Berlin Jumapili.

Xavi Simons hapo awali aliipatia Uholanzi bao la kuongoza dakika ya saba kwa shuti kali la mbali kabla ya Harry Kane kusawazisha dakika ya 18 kwa mkwaju wa penalti iliotolewa baada ya marudio ya VAR kufuatia Denzel Dumfries kumchezea rafu nahodha huyo wa England.

Southgate, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa England mwaka 2016, sasa amewaongoza hadi robo fainali, nusu fainali na fainali mbili katika michuano yake minne mikubwa akiwa kama kocha wa timu hiyo.

England haijawahi kufika fainali kubwa katika ardhi ya kigeni, baada ya kupoteza fainali ya mwisho ya Euro kwenye Uwanja wa Wembley kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Italia.

Mafanikio yao pekee ya mashindano makubwa yalikuja kwa kubeba Kombe la Dunia mwaka 1966, tena kwenye ardhi yao.


Alipoulizwa aliweka wapi mafanikio ya Jumatano katika kipindi chake cha miaka nane, Southgate aliiambia ITV, „Ndio, nadhani lazima liwe bora zaidi. Ni alama nyingine, lakini jinsi tulivyocheza pia, tulicheza vizuri sana katika muda wote wa mchezo. „

Southgate amekabiliwa na shutuma kali za kibinafsi kwa kile ambacho wengi wanaamini kuwa ni mbinu ya tahadhari kupita kiasi huku timu yake ikizomewa mara mbili mapema kwenye michuano hiyo.

„Sote tunataka kupendwa, sivyo? Unapofanya jambo kwa ajili ya nchi yako na wewe ni Mwingereza mwenye fahari, wakati haujisikii kwamba nyuma na yote unayosoma ni ukosoaji, ni ngumu,“ alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari.

„Kuweza kusherehekea fainali ya pili ni maalum sana. Hasa mashabiki wanaosafiri na timu. Msaada wetu wa kusafiri ni wa kushangaza, fedha wanazotumia, kujitolea kufanya hivyo, kuweza kuwapa usiku kama huu, hii ina maana kubwa.

# Coutinho apelekwa kwa mkopo Vasco da Gama



**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imethibitisha kumtoa mchezaji Phillipe Coutinho kwa mkopo kwenda timu ya Vasco Da Gama ya nchini Brazil.

Mbrazili huyo anarejea kukipiga katika nchi yake baada ya kucheza klabu ya Al Duhail msimu uliopita.

Baada ya kujiunga kwa mkopo Aston Villa Januari mwaka 2022, Coutinho alisaini mkataba wa kudumu klabuni hapo ambapo ameichezea michezo 43 na kufunga mabao 6.

Kabla ya hapo, Coutinho alicheza kwa mafanikio akiwa na Liverpool kabla ya kutimkia Barcelona kwa ada kubwa lakini hakuweza kuonesha kiwango bora na hivyo kutimkia Bayern Munich kwa mkopo na kisha Aston Villa.

# Colombia yatinga fainali Copa America kwa fujo

**NORTH CAROLINA,** Marekani

JAMES Rodriguez alitoa pasi yake ya sita ya mabao katika michuano ya Copa America na kuisaidia Colombia iliyokuwa na wachezaji 10 kuwalaza Uruguay bao 1-0 mjini Charlotte, North Carolina, Jumatano na kutinga fainali watakayocheza dhidi ya Argentina, kabla ya usiku huo kuingia kwenye fujo huku wachezaji wakizozana na mashabiki.

Argentina iliishinda Canada 2-0 katika nusu fainali ya kwanza Jumanne na kujikatia tiketi ya kucheza fainali Jumapili huko Miami Gardens, Florida.

Ushindi wa Colombia siku ya Jumatano ulimaanisha kuendeleza mbio zao za kutoshindwa hadi kufikia rekodi ya michezo 28, tangu ilipopoteza mbele ya Argentina Februari 2022.

Katika mechi hiyo yenye utata iliyojumuisha kadi saba za njano na nyekundu moja, wachezaji wa timu zote mbili walitunishiana misuli uwanjani.

Darwin Nunez na takriban wachezaji wote wa Uruguay waliingia kwenye mzozo na mashabiki.

Picha za video zilionesha Nunez akimpiga shabiki aliyevaa jezi ya timu ya Colombia.

Jefferson Lerma alifunga bao pekee mbele ya umati wa watu 70,644 waliokuwa wakiiunga mkono Colombia kwenye Uwanja wa Bank of America alipounganisha kwa kichwa mpira wa kona kutoka kwa James dakika ya 39.

James anakuwa mchezaji wa kwanza wa Amerika Kusini kutoa asisti sita katika mchuano mmoja mkubwa tangu Pele alipoichezea Brazil katika Kombe la Dunia la mwaka 1970.

Kazi ya Colombia kulinda ushindi wao iliingia kwenye wasiwasi pale mlinzi wao Daniel Muñoz alipotolewa kwa kadi nyekundu kipindi cha kwanza baada ya kupokea kadi ya pili ya njano kwa kumpiga kiwiko Manuel Ugarte wa Uruguay.

Muñoz alipokea kadi yake ya kwanza ya njano kutoka kwa mwamuzi wa Mexico César Ramos dakika ya 31 kwa kumpiga kizembe Maximiliano Araújo.

Mshambuliaji wa Liverpool, Núñez alishindwa kutumia fursa nyingi za kipindi cha kwanza, huku kipa wa Colombia, Camilo Vargas, akilazimika kuokoa hatari ya Nicolas de la Cruz dakika ya 68.

Luis Suárez aliyetokea benchi, nahodha wa zamani wa Uruguay aliyefunga mabao 68, aligonga nje ya nguzo kwa shuti la dakika ya 71 huku Uruguay ikihangaika kupata ushindi dhidi ya wachezaji 10.

Mateus Uribe wa Colombia, mchezaji mwingine mdogo kwenye michuano hiyo alipiga shuti la wazi dakika ya 88 na kugonga mwamba.

HABARI MICHEZO

## Gamondi atoa kauli nzito

INATOKA UK. 24

yeye kama mwalimu ndiye anayejua atawatumia vipi na si mtu mwingine yoyote, na katika timu lazima kuwe na uwiano.

"Watu wanawaza kutaka fulani na fulani wacheze, hapana siwezi kufanya hivyo, unajua kocha anatakiwa kuifanya timu kuwa na uwiano, msimu uliopita tulicheza mechi 50, hivyo tuna michezo mingi sana msimu ujao, hivyo kuna muda atacheza Aziz Ki, wakati mwingine Chama, au Dube, kuna muda hawatacheza kwa sababu huu ni mpira, ninachofurahi kama kocha ni kuwa na machaguo mengi, nina uhakika kiwango chetu kitaongezeka hasa kwenye michezo ya kimataifa," alisema Gamondi.

## Yanga SC kuanza na Warundi CAF..

INATOKA UK. 24

Katika droo hiyo iliyochezeshwa jana alasiri Makao Makuu ya CAF, Cairo, Misri, timu zote za Tanzania zitaanzia hatua ya awali isipokuwa Simba inayoshiriki Kombe la Shirikisho itaanzia hatua ya kwanza kwa kukusubiri mshindi kwenye mchezo kati ya Uhamiaji FC ya Zanzibar na mwakilishi kutoka Libya ambaye bado hajapatikana.

Katika kombe hilo, Coastal Union yenyewe itacheza na FC Bravos do Maquis ya Angola katika hatua ya awali.

Mwakilishi mwingine wa Zanzibar michuano hiyo, JKU inayoshiriki Ligi ya mabingwa yenyewe imepangwa kucheza na Pyramids ya Misri na mshindi katika mchezo huo atacheza na mshindi kati ya Azam FC na APR.

Michezo ya marudiano imepangwa kuchezwa kati ya Agosti 23 mpaka Agosti 25.

Endapo Yanga atafanikiwa kumuondoa kwenye michuano hiyo Vital'O, ataumana na mshindi kati ya Villa SC ya Uganda watakaocheza na Commercial Sports ya Ethiopia.

Wakati droo hiyo inatoka tayari timu za Tanzania zimeshaanza maandalizi ya kuelekea kwenye msimu mpya, ambapo Yanga juzi ilianza mazoezi kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam, chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ikitarajia pia kwenda nchini Afrika Kusini kucheza mechi ya Kombe la Toyota dhidi ya Kaizer Chiefs utakaopigwa Julai 28.

Azam FC yenyewe iko Zanzibar na leo inatarajiwa kukipiga na Zimamoto kwenye mchezo wa kirafiki, huku ikiwa kwenye maandalizi ya kuelekea nchini Morocco kuweka kambi.

Simba ambayo itasubiri hadi Septemba kucheza michuano hiyo ya CAF, nayo imeanza maandalizi ambapo tayari ipo nchini Misri kwenye jiji la Ismailia ikijifua kwa ajili ya michuano hiyo na Ligi Kuu.

# AWESU, KIJILI KUFUNGA USAJILI MPYA SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI Awesu Awesu kutoka KMC na Kelvin Kijili wa Singida Blach Stars, wametajwa kuwa ndiyo watakaofunga usajili msimu huu kunda kikosi cha Simba.

Habari kutoka ndani ya Simba zinasema kuwa taratibu chache zinamaliziwa kuweza kuwatangaza wachezaji hao ambao nao baadaye watakwea pipa kwenda kuungana na wenzao nchini Misri ambako imeweka kambi kwa ajili ya msimu ujao wa michuano ya kitaifa na kimataifa.

„Ni kweli, tunaendelea na mazungumzo ya mwisho, dirisha la usajili bado lipo wazi, na hawa ndiyo watatufungia dirisha, hapo tutakuwa tumeshakamilisha kazi," kilisema chanzo ndani ya klabu hiyo.

Awesu anakwenda kuongeza nguvu kwenye eneo la kiungo mshambuliaji, huku Kijili akienda kupeleka changamoto kwa beki wa kulia, Shomari Kapombe pamoja na Israel Mwenda, huku David Kameta akiondoka kwa mkopo.

„Tumesajili beki wa kushoto Valentin Nouma kwenda kumpa changamoto Tshabalala (Mohamed Hussein), sasa ule upande wa Kapombe ulikuwa bado, tulikaa na kuona Kijili anafaa, na Awesu ametuonyesha kuwa ni mmoja wa wachezaji wa Kitanzania ambao ana uwezo mkubwa, anajitambua na mwenye nidhamu, tumeamua kumsajili," kiliongezea kusema chanzo hicho.

Ingawa hakutaja majina ya wachezaji hao, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally alikiri kuna maingizo mengine ya wachezaji wachache ndani ya kikosi.

„Tumefanya usajili kwa asilimia 98, kuna wachezaji wachache kama wawili watatu ambao watakuja kukamilisha kikosi, na kuna ‚thank you' kama nne zinakuja, na niwaambie kuwa kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi, kikosi kinaandaliwa Misri," alisema Ahmed.

Iwapo wachezaji hao watasajiliwa, Simba itakuwa imesajili wachezaji saba wapya wazawa kuelekea msimu ujao.

Tayari imeshawatia mikononi, Lameck Lawi kutoka Coastal Union, Abdulrazack Hamza wa Super Sports ya Afrika Kusini, Valentino Mashaka, akitokea Geita Gold, Omari Omari aliyekuwa akikipiga Mashujaa FC na Yusuph Kagoma kutoka Singida Black Stars.

Pia imesajiliwa wachezaji saba wa kigeni ambao ni Nouma, kutoka FC Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jushua Mutale kutoka Power Dynamos ya Zambia, Steven Mukwala kutoka Asante Kotoko ya Ghana, Jean Charles Ahoa kutoka, Stella Adjame ya Ivory Coast, Debora Fernandes Mavambo kutoka Mutondo Stars ya Zambia, Augustine Okajepha, kutoka Rivers United ya Nigeria na Karaboue Chamou, akitokea klabu ya Racing Club d'Abidjan ya Ivory Coast.

Wakati huo huo, klabu hiyo imekanusha kuwa itamtoa kwa mkopo mchezaji wake Hussein Kazi, ambaye awali ilidaiwa hajasafiri na kikosi.

„Kazi yupo kikosini, kumekuwa na maneno maneno mengi kuwa amerudishwa, hayana ukweli, yeye yupo Ismailia akiendelea na mazoezi na wenzake," alisema Ahmed.



Wachezaji wa klabu ya Al Hilal Omdurman wakishangilia moja ya goli walilofunga juzi usiku kwenye mchezo dhidi ya ASAS ya Djibout wakati wa michuano ya Kombe la Kagame kwenye uwanja wa Azam Complex. Al Hilal walishinda mabao 2-0. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Bongo Movie wampongeza Rais Samia safari ya Korea

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya kurejea nchini, Wasanii wa filamu na Tamthilia wampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kugharamia safari yao ya Korea iliyokuwa na lengo la kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu sekta ya sanaa ya filamu na tamthilia duniani.

Wakizungumza na mwandishi wa habari jana baada ya kurejea kutoka Korea walipokwenda huko tangu Julai mosi, walisema wamejifunza namna ya kufanya kazi zao za kisanii kama njia ya kujiletea maendeleo na kukuza sekta hiyo nchini Tanzania.

Baadhi ya wasanii waliokwenda Korea ambao walizungumza na waandishi wa habari na kumshukuru Rais Samia, ni pamoja na Steve Nyerere kama Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Idris Sultan, Wema Sepetu, Irene Uwoya, Monalisa, Irene Paul, Gertrude Mwita na Godliver Gordian.

Wasanii hao kwa umoja wao wamempongeza Rais Samia kwa kuwapa fursa kwenda kujifunza zaidi kuhusu sanaa na wanaamini walichojifunza huko kitawasaidia katika shughuli zao.

Kwa upande wa maboresho ya sekta hiyo, wasanii hao waliitaka serikali kuweka mikakati zaidi kugharamia utendaji kazi wa Sanaa wa Tanzania kama walivyofanya Korea kwa kuweka bajeti ya uandaaji wa filamu zao hali iliyoibua na kuendeleza sekta hiyo.

„Ili kuwa wakubwa na kutangaza makampuni na viwanda vyetu, watumike wasanii wa ndani kutangaza shughuli zao," alisema Steve,

Safari ya wasanii hao imekuja wakati ambao Rais Samia alitangaza neema kubwa kwa wasanii ya kugharamia safari zao pindi atakapokuwa na ziara za kikazi nje ya nchi.

Michezo

Ijumaa Julai 12, 2024

Nipashe



Palhinha atua rasmi Bayern Munich

UK. 21



Mshambuliaji wa timu ya taifa ya England, Ollie Watkins (kushoto) akipiga shuti kufunga bao la pili na la ushindi mbele ya beki wa Uholanzi kwenye mchezo wa nusu fainali ya Euro juzi usiku. England ilishinda mabao 2-1 na kutinga fainali ya michuano hiyo  watakayocheza na Hispania Jumapili. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI ATOA KAULI NZITO

## ●●● Asema hatoangalia jina la mtu kwenye kupanga kikosi chake cha kwanza bali....

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ametahadharisha kuwa kuelekea msimu ujao atapanga kikosi chake kutokana na kiwango cha mchezaji na jinsi anavyojituma kwenye mazoezi na si jina la mtu.

**Kauli hiyo imekuja baada ya kuwa na maswali kwa mashabiki na wanachama wa timu hiyo wakifikiria nani ataanza kwenye kikosi cha kwanza kutokana na aina ya usajili uliofanywa kukiimarisha kikosi hicho.**

Yanga imewaongeza kikosini, kiungo Clatous Chama aliyeachana na Simba baada ya mkataba wake kumalizika na mshambuliaji Prince Dube ambaye aliamua kuvunja mkataba wake na klabu ya Azam FC.

Akizungumza mara baada ya mazoezi ya kwanza ya kikosi hicho juzi kwenye ufukwe wa bahari maeneo ya Coco, Miguel, alisema kama kuna mchezaji anatarajia kucheza kwa sababu ya jina lake asahau, badala yake atapanga kikosi kutokana na kile kilichoonyeshwa kwenye uwanja wa mazoezi, pamoja na kiwango anachokionyesha uwanjani.

Gamondi alisema,  amefurahi kuona kikosi chake kimeongezewa wachezaji mahiri kiasi cha kutompa tabu kupanga kikosi.

„Kila kocha anaona furaha kuwa na wachezaji bora, angalia kuna Chama, Pacome (Zouzoua), Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Mudathir (Yahaya), Khalid Aucho, ila kuwapanga inategemea na mpinzani unayoenda kucheza naye na kiwango chake, kwangu mimi hakuna kucheza kwa sababu ya jina bali kiwango, nataka kila mchezaji aonyeshe kiwango chake ili kuwa katika kikosi cha kwanza,“ alisema Kocha huyo.

Hata hivyo, amewataka mashabiki pamoja na wapenzi wa timu hiyo kuwa na subira na wachezaji wapya kwani pamoja na uwezo wao, wanahitaji muda ili waweze kuonyesha kile walichokuwa wakikifanya katika timu walizotoka.

„Tunatakiwa kuwa wavumilivu kwa sababu wanatakiwa kujua mbinu zetu za kimchezo na kufahamiana na wenzao, nafikiri watu wasiwe na haraka kuwaona wachezaji wapya wakicheza vile wanavyotaka wao, kwani katika soka baadhi ya wachezaji hawana muda wa kusubiri, ukiwaweka tu uwanjani wanacheza vizuri, lakini wengine wanahitaji muda,“ alisema Gamondi.

Kuhusu mfumo wa uchezaji, alisema

INAENDELEA UK. 23

## Yanga SC kuanza na Warundi CAF, Simba kusubiri Uhamiaji, Walibya

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la soka Afrika (CAF) jana lilichezesha droo ya timu zitakazokutana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ambapo wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo tayari wamewafahamu wapinzani wao.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, mabingwa wa soka Tanzania, Yanga wenyewe wataumana na Mabingwa wa Burundi, Vital'O Club huku Azam FC ikipangwa kucheza na APR ya Rwanda ambapo Yanga wataanzia ugenini huku Azam wakianzia nyumbani kati ya Agosti 16 na 18.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >